
**MAKALA MAALUM**
Hii ndiyo maana halisi ya Pasaka UK. 4

**Mwanafunzi** aliyeumwa na nyoka atoka hospitalini
UKURASA 5



**MAKALA MAISHA**
Kulikoni kasi wake kukimbia waume zao?
UKURASA 11



JAZA NYWELE KIASILI
UKURASA 14


# Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Machi 31, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • No. 0581632
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Mambo makubwa uwekezaji SGR

• **Wawekezaji** binafsi ruksa kuingiza vichwa, mabehewa, ufanisi bandari kupaa kufuata... *uk. 2*



Masanja Kadogosa



## Ole Sendeka anusurika kifo, afunguka alivyokwepa risasi
UKURASA 3



## Madaktari, wauguzi wawekwa matatani kifo cha mjamzito
UKURASA 3

**MICHEZO** AL AHLY YAVUNJA REKODI YA SIMBA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Mambo makubwa uwekezaji SGR

**Na Mwandishi Wetu**

YAJAYO yanafurahisha. Hivyo ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na uwekezaji mkubwa unaoendelea katika reli ya kiwango cha kimataifa (SGR) ambayo ujenzi wake unaendelea kwa kasi katika maeneo mbalimbali.

Kazi hiyo inafanyika kwa awamu kulingana na ilivyogawanywa katika vipande huku Dar es Salaam hadi Morogoro kikiwa kimekamilika na wakati wowote wananchi wataanza kutumia usafiri huo ambao unatumia muda mfupi na majaribio ya treni yameshaanza.

Kwa kawaida, usafiri wa mabasi kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro ni takriban saa nne au zaidi lakini kwa reli ya SGR ni dakika 90 tu na itasimama vituo vyote ambavyo ni Dar es Salaam, Pugu, Soga, Kwala, Ngerengere na Morogoro. Muda huo unaonyesha kuwapo kwa faida kubwa kwa usafiri wa haraka na wa uhakika.

Muda unaotumika katika usafiri huo ni tofauti na reli ya kawaida (MGR) ambao unatumia saa tano na nusu hadi sita na nusu. Treni ya kawaida (ordinary) kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro, kwa mfano, unatumia saa sita na nusu wakati ile ya Deluxe inatumia saa tano na nusu.

Usafiri huo wa treni ya SGR ni wa muhimu kwa kuwa utarahisisha uafirishaji wa abiria na mizigo, hivyo kupunguza muda na hasara ambazo wananchi na wafanyabiashara wanazipata kutokana na kutumia muda mrefu kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

Wakati wa hafla ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa kipande cha Tabora mpaka Isaka Januari, 2023 makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alisema: "Lengo la serikali (kutokana na mradi wa SGR) ni kuwapunguzia wananchi muda wa safari na gharama za bidhaa kutokana na gharama za usafirishaji wa malighafi na bidhaa ili kuboresha maisha."

Ujenzi wa kipande hicho unatarajiwa kufanyika kwa miezi 42 na kukamilika Machi, 2026 kwa gharama ya Sh. Trilioni 2.6.

Mbali na vipande hivyo, kipande cha Morogoro hadi Dodoma, ujenzi wake umefikia asilimia 97 na majaribio yameshaanza na vingine ambavyo ujenzi wake umeanza au unaendelea na kiwango cha asilimia ni Isaka -Mwanza (54.01), Tabora- Isaka (5.44), Makutupora - Tabora (14).

Ujenzi wa Tabora hadi Kigoma, unatarajiwa kuanza baada ya kumalizika kwa mvua za masika wakati cha Uvinza hadi Msongati nchini Burudi tayari mkandarasi ameshapatikana.




Mbali na vipande hivyo, kazi hiyo pia inatarajia kufanyika katika kanda ya Kaskazini, kwa maana ya kutoka Ruvu Junction hadi Tanga- Moshi na Arusha na baadaye kufika Musoma. Reli hiyo ya SGR inatarajiwa pia kujengwa kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay mkoani Ruvuma.

**YAJAYO YANAFURAHISHA**

Kwa jicho la kawaida, watu wanafikiria katika unafuu wa usafiri na usafirishaji kutoka sehemu moja hadi nyingine katika maeneo ya mredi huo lakini kuna mambo makubwa yanayotarajiwa ikiwamo kufuka kwa uchumi na kuongeza mapato katika sekta mbalimbali.

Akizungumza hivi karibuni mafanikio ya mradi huo hasa katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, alisema kuna mafanikio makubwa kupitia mradi huo ambao hadi sasa umetumia fedha nyingi katika utekelezaji wake.

"Watu wanazungumza kwamba mradi unatumia fedha nyingi. Ni kweli lakini tusiangalie katika fedha zinazotumika bali faida zake. Kubwa Zaidi, mradi huu utafungua uchumi wa nchi kwa kiasi kikubwa. Kwa kutambua hilo, ndiyo maana Rais (Samia) amekuwa anatafuta fedha na kuzielekeza katika mradi. Lengo ni kuleta maendeleo ya wananchi na kuinua uchumi.

"Lengo ni kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha uchumi kwa nchi tunazopakana nazo ambazo hazina bandari na zinategemea bandari zetu wa ajili ya uagizaji na usafirishaji wa mizigo yao kutoka nje. Reli ya kwenda Mwanza, kwa mfano, tunalenga soko la Uganda," alisema. Kuwapo kwa usafiri huo utaiwezesha Uganda kupata mizigo inayopitia bandari ya Dar es Salaam kwa muda mfupi na kwa gharama nafuu. Kwa mujibu wa Kadogosa, Kampala pekee hupokea tani milioni nane za mizigo kwa mwaka.

"Kwa hiyo mizigo ikifika Mwanza itakwenda na kufika haraka. Pia kutakuwa na fursa ya bandari kavu Port Bell na Jinja. Hali hiyo ipapunguza gharama kwakiasi kikubwa. Kigoma pia itaweaesha mizigo kufika Kelemie (Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo) na kurahisisha mizigo kufika kwa haraka mashariki mwa Congo kutoka Kalemie hadi Lubumbashi," alisema.

Kadogosa alibainisha kuwa malori ya mizigo kutoka Dar es Dar es Salaam - Bukavu hadi Goma (DRC) yanatumia siku 15. Hali hiyo, alisema inasababisha gharama kubwa kwa mzigo kufika na matokeo yake gharama za bidhaa zinakuwa juu na wanaoumia ni watumiaji kutokana na kupandishwa kwa bei za bidhaa husika.

"Baada la reli kukamilika, Dar es Salaam hadi Bukavu mzigo utafika ndani ya saa 48 (siku mbili). Hii itapunguza gharama sana. Kutoka bandari ya Durban (Afrika Kusini) hadi Katanga (DRC) gharama ya kusafirisha kontena la futi 40 ni dola za Marekani 15,000 (Sh. milioni 37.5) lakini baada ya reli, gharama yake itashuka hadi chini ya Dola 5000 (takribani Sh. milioni 12.5).

**UFANISI WA BANDARI**

Licha ya kunufaisha mataifa mengine, Mkurugenzi Mkuu alisema kukamilika kwa SGR kutafungua milango ya uchumi kwa bandari ya Dar es Salaam na baadaye Tanga na Mtwara kuongeza ufanisi.

"Tunatambua kwamba bandari yetu ni lango la uchumi kwa Tanzania na nchi za jirani. Kwa hiyo reli hii itawezesha bandari yetu hasa ya Dar es Salaam kuongeza ufanisi kwa kupokea na kuondoa mizigo kwa haraka.

"Kazi kubwa ya bandari ni kuza sehemu kwa ajili ya kuweka mizigo kabla ya kuondolewa na kupelekwa inakohusika. Sasa kuwapo kwa reli ya kisasa kutafungua bandari zetu na kuwa na ufanisi na makusanyo yataongezeka mara mbili hadi tatu tofauti na sasa.

"Mizigo itakuwa inaingia na kutoka na kwa vile kutakuwa na usafiri wa urahisi na wa haraka kupitia reli, meli zitaongezeka kwa kushusha mizigo kwa muda mfupi tofauti na hali iliyopo sasa," alibainisha.

"Lakini jambo la muhimu ni kwamba reli hii haiwezi kuwa na ufanisi kama sekta binafsi haishashirikishwa ipasavyo. Watanzania wafanye biashara na nchi zingine kupitia reli hii. Kwa kufanya hivyo, ndipo itajulikana reli hii ina maana gani kwa Watanzania. Tunaweza kuwaachia wenzetu wakaitumia ipasavyo na tukawa watazamaji," alisisitiza.

Sambamba na hilo, kiongozi huyo alisema kwa sasa mizigo mingi ya ndani na nje inasafirishwa kwa kutumia malori ambayo licha ya kuwa na gharama kubwa pia husababisha uharibifu wa miundombinu hasa barabara. Kwa mantiki hiyo, ukio wa reli ya kisasa itawezesha pia kulinda miundombinu hiyo kwa sababu mizigo mingi itasafirishwa kwa kutumia reli isipokuwa ile ambayo inakwenda sehemu ambazo hazina reli.

Pia alisema msongamano wa magari kati ya Morogoro hadi Dar es Salaam utapungua kutokana na kujengwa kwa bandari kavu eneo la Kwala mkoani Pwani. Bandari hiyo itakuwa maalumu kwa ajili ya mizigo kutoka bandari ya Dar es Salaam hadi hapo kicha kuchukuliwa na malori kwenda maeneo yasiyo na reli.

"Malori ya mizigo yatakuwa yanaishia Kwala badala ya kujazana katika bandari ya Dar es Salaam na hii itapunguza sana foleni katika baadhi ya maeneo Dar es Salaam. Mizigo itakuwa itakuwa inatoka bandarini hadi Kwala, pale ndipo malori yatakuwa yanachukua na kupeleka kunakohusika.

"Lakini pia tuelewe kuwa yale malori tunayoyaona yakienda Mwanza, Dodoma, Shinyanga na kwingineko yatakuwa mwisho kwa sababu mizigo itasafirishwa kwa treni kwenda huko. Kwa hiyo barabara zetu pia zitadumu na hata ajali pia zitapungua ambazo husababishwa na malori haya," alisema Kadogosa.

**WAWEKEZAJI BINAFSI**

Kadogosa alihojiwa kama wawekezaji na wafanyabiashara wanaruhusiwa kuingiza mabahewa yao kama ilivyo katika reli ya sasa.

"Serikali kupitia TRC inamiliki miundombinu ya reli na mabehewa na vichwa vya treni kwa ajili ya uendeshaji. Hii haimaanishi kwamba kwa kufanya hivyo itatosheleza mahitaji ya huduma hasa usafirishaji wa mizigo.

"Kama ilivyo kwenye reli ya zamani, kuna wawekezaji binafsi kama MeTL, Bakhresa, Azania na Uganda Railway. Pia kuna vichwa vya sekta binafsi katika reli hii ya zamani.

Kwa reli mpya pia wawekezaji binafsi wataruhusiwa kuingiza mabehewa yao na vichwa. Suala si kuingiza tu bali yawe na viwango na vipimo vinavyotakiwa kulinanga na saizi ye reli na uzito wake. Watapata leseni kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) na kanuni zinaandaliwa pamoja na operational manual (kitini cha uendeshaji) kitakamilika ifikapo Mei, mwaka huu," alisema.

**MANUFAA KWA WAZAWA**

Kuna msemo kwamba 'mgeni njoo mwenyeji apone'. Ndivyo ilivyo kwenye mradi wa ujenzi wa SGR kutokana na manufaa makubwa ambayo wameyapata.

Moja ya manufaa hayo ni ajira kwa wazawa. Kadogosa alisema tangu kuanza kwa mradi huo, ajira za moja kwa moja 31,000 zimepatikana na zingine 150,000 ambazo si za moja kwa moja.

"Ajira hizi zitachangia ukuaji wa sekta zingine kama kilimo, ufugaji na biashara," alisema.

Manufaa mengi yametokana na wafanyakazi walioajiriwa ndani ya TRC, makandarasi na watoa huduma mbalimbali. Lakini pia tunatarajia ajira nyingi kupatikana kwa uwapo wa bandari kavu Kwala. Viwanda vitajengwa na kutakuwa na shughuli mbalimbali katika eneo lile. Mradi hii pia itachochea kwa mujibu wa Kadogosa wazalishaji wa ndani kupata fursa ya kuuza vifaa vya ujenzi kama nondo na saruji kwa ajili ya ujenzi wa reli. Alibainisha kuwa hakuna kifaa chochote cha ujenzi, hasa vile vinavyopatikana nchini, kilichoagizwa toka nje kwa ajili ya mradi.

"Kupitia mradi huu wenye viwanda vya nondo na saruji vilinufaika na vinaendelea kunufaika kwa kiasi kikubwa kupitia mradi huu. Kuna kipindi itakumbukwa kulikuwa na kilio kikubwa cha uhaba wa saruji. Haikuwekwa wazi sababu ya uhaba huo lakini ukweli ni kwamba saruji nyingi ilipelekwa kwenye ujenzi wa SGR," alisema.

Anatoa wito kwa wazalishaji wa ndani kwamba waendelee kuchangamkia fursa hiyo kwa kuwa kazi ya ujenzi wa reli hiyo bado ni mbichi na inahitaji vifaa vingi.



Mfanyabiashara wa mihogo akiipanga kuvutia wateja kandokando ya barabara ya Chanika Dar es Salaam katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhan ambapo fungu moja linauzwa kwa Sh.2000. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Madaktari, wauguzi matatani kifo mjamzito

**Na Oscar Assenga,** TANGA

MKUU wa Wilaya ya Tanga, James Kaji, amemwagiza Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Dk. Fedrick Sagamiko, kuwasimamisha kazi watumishi watano wakiwamo madaktari wawili kutoka Kituo cha Afya Mikanjuni, wanaotuhumiwa kusababisha kifo cha mjamzito, Fatma Suleiman (36).

Fatma ambaye ni mkazi wa Magaoni inadaiwa Machi 28, mwaka huu, alifanyiwa upasuaji na kuwekewa damu kinyume cha utaratibu, baada ya kwenda kituoni hapo kwa ajili ya kujifungua. Watumishi wengine ni wauguzi watatu.

Aliwataja wanaotakiwa kusimamishwa kazi ili kupisha uchunguzi kuwa ni madaktari Hamisi Mohamed na Andrew Kidee na wauguzi watatu ambao ni Fadhia Hoza, Restituta Deusdedit na Muya Mhando.

Kaji alisema baada ya vipimo vya awali ilibainika kwamba, mama huyo alikuwa akihitaji kufanyiwa upasuaji.

Alisema baada ya upasuaji huo mama na mtoto walikuwa kwenye hali nzuri, walipelekwa wodini kwa ajili ya uangalizi, huku wakisubiri kupewa ruhusa ya kurudi nyumbani.

Alisema mama huyo akiwa wodini baadaye muuguzi aliyekuwa zamu alifika na kumwekea damu ambayo ilikuwa haiendani na kundi lake (damu iliyotakiwa kuwekwa kwa mgonjwa mwingine) jambo ambalo lilisababisha kifo chake.

"Nimewaita kuzungumzia taarifa ya kifo cha Fatma Suleiman (36), mkazi wa Magaoni kilichotokea Machi 28, mwaka huu. "Fatma alikuwa ni mjamzito na alilazwa Kituo cha afya Mikanjuni Machi 28 mwaka huu saa 10 alfariji kwa tatizo la uchungu, aliendelea kuwa chini ya uangalizi wa madaktari na muuguzi," alisema.

Alisema daktari wa zamu alipofika saa tisa mchana alionekana mama huyo mjamzito ana changamoto uchungu pingamizi na mtoto alikuwa ameanza kupata changamoto, hivyo madaktari waliamua kumfanyia upasuaji.

Kwa mujibu wa Kaji, mgonjwa alifanyiwa upasuaji na kupata mtoto wa kike aliyekuwa na uzito wa kilo 3.4 na hakukuwa na changamoto yoyote kwa mama wala mtoto na katika wodi hiyo aliyolazwa kulikuwa na mgonjwa mwenye uhitaji wa kuwekewa damu na ilikuwa imeandaliwa na muuguzi aliyekuwa zamu.

Kaji alisema muuguzi huyo alimwekea Fatma damu ambayo ilikuwa haihitajiki kwake bali kwa mgonjwa mwingine.

"Niendelee kutoa rai kwa wauguzi na madaktari kuwa makini wakati wa utoaji wa huduma ili kuepukana na changamoto mbalimbali ikiwamo ya kusababisha vifo," alionya.

**SABABU ZA KIFO**

Kaji alisema kifo hicho kimetokea kwa uzembe kwa kuwekewa damu ambayo hakuwa na uhitaji nayo na kupata mzio mkali (Allergic Reaction) na kumsababishia kifo.

# Ole Sendeka anusurika kifo, afunguka alivyokwepa risasi

**Na Mwandishi Wetu,** KITETO

MBUNGE wa Simanjiro (CCM) mkoani Manyara, Christopher Ole Sendeka, amefunguka alivyojinusuru na dereva wake kushambuliwa kwa risasi kuwa ni baada ya kujibu mapigo.

Akisimulia shambulio hilo lilivyotokea juzi ambalo tayari Jeshi la Polisi limepeleka timu ya wataalam wa uchunguzi wa matukio kutoka makao makuu ya polisi, Ole Sendeka alisema kilichomnusuru ni ujasiri wake wa kuamua kuwatisha kwa kujibu mashambulizi.

Shambulio hilo lilitokea juzi saa 12:45 jioni katika Kijiji cha Ngabolo, wilaya ya Kiteto, mkoani Manyara.

"Kulikuwa na gari ambalo lilikuwa linanifuatilia kwa nyuma, tukawapisha kidogo wapite kulia. Walipofika usawa wetu, wakaanza kumimina risasi upande wa dereva na baada ya hapo, wakavuta kwenda mbele halafu wakaanza kuzipiga za usoni.

"Na sisi tukakata kona kugeuza. Na mimi nikaanza kupigapiga (risasi) za juu pale kuwatishiatishia, ndipo tukafanikiwa kugeuza na kuondoka. Walikuwa na silaha kubwa na silaha ndogo. Hakuna aliyepata madhara na tulikuwa mimi na dereva wangu. Ni gari tu ndilo wamelichakaza, wamelipigapiga.

"Hatujazihesabu (risasi) lakini zipo risasi moja, mbili, tatu, nne; kama nne hivi au tano zipo waziwazi (matundu ya risasi yanaonekana kwenye gari)," alisema.

Hata hivyo, Ole Sendeka alipoulizwa kama kuna sababu yoyote anayohisi kwa yeye kushambuliwa kwa risasi, alisema bado hawezi kusema jambo kwa wakati huu na wala si rahisi kujua sura za waliohusika katika tukio hilo.

Katika taarifa kwa umma iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi la Polisi Nchini, Naibu Kamishna (DCP) David Misime alisema jeshi hilo limepokea taarifa ya Mbunge wa Simanjiro.

Misime alisema tayari jeshi limepeleka timu ya wataalam wa uchunguzi wa matukio yaliyohusisha matumizi ya risasi kutoka Makao Makuu ya Polisi, kuchunguza ili kubaini waliohusika ni kina nani na madhumuni au kusudio lao lilikuwa nini.

Alisisitiza kuwa polisi wanafuatilia tukio hilo kwa ukaribu na baada ya kulichunguza taarifa kamili itatolewa.

# Waziri Mkuu amfagilia Samia utekelezaji miradi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan, ni kinara na kielelezo cha utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayoigusa jamii ya watanzania.

Majaliwa amesema maono na misingi iliyojengwa na Rais Samia imewezesha serikali kutekeleza mipango mbalimbali ya maendeleo ikiwamo miradi ya kimkakati na kuimarisha utoaji wa huduma za jamii.

Akizungumza katika kongamano la Maadhimisho ya miaka mitatu ya Rais Samia lililofanyika mkoani Mwanza jana, Majaliwa alisema serikali imetekeleza miradi ya usafiri katika Maziwa Makuu.

"Serikali imefanya mageuzi makubwa katika sekta ya usafiri na usafirishaji kwa kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya kuimarisha usafiri wa anga, usafirishaji kwa njia ya reli, barabara na usafiri katika bahari na maziwa makuu," alisema.

Alisema miongoni mwa miradi ni mradi wa ujenzi wa meli ya Mv. Mwanza Hapa Kazi Tu yenye uwezo wa kubeba abiria 1200, tani 400 za mizigo, magari madogo 20 na malori matatu na hadi sasa umefikia asilimia 94 ya ujenzi wake.

Alisema serikali pia imefanya maboresho katika bandari na kuongeza ufanisi wa utoaji huduma katika bandari hizo ikiwamo bandari kwenye Ziwa Victoria.

Pia alisema katika kuimarisha sekta ya kilimo, serikali imeendelea kuboresha usimamizi na utoaji wa huduma kwa kuongeza bajeti katika Wizara ya Kilimo.

"Serikali imeweka msisitizo katika usimamizi wa zao la pamba ikiwamo kuongeza thamani ya zao hili. Nitoe wito kwa wakulima wa zao hili, kuongeza uzalishaji ili mahitaji tuliyo nayo yaendane na uhitaji uliopo," aliagiza.

Kadhalika, alisema serikali inaendelea na ujenzi wa mradi wa Bandari ya Uvuvi pamoja na kutoa zana bora, pembejeo na vifaa muhimu vitakavyowawezesha kufanya shughuli zao kwa ufanisi, lengo ni sekta hiyo kuchangia zaidi katika Pato la Taifa na uchumi wa mtu mmoja mmoja.

"Zimenunuliwa na kusambaza boti 160 za kisasa za uvuvi zenye thamani ya Sh. bilioni 11.5 kwa vyama vya ushirika wa wavuvi, watu binafsi na vikundi vya wavuvi katika halmashauri 58," alisema.

Katika hatua nyingine, Majaliwa ametoa wito kwa wafanyabiashara kutumia fursa za uwekezaji zilizowekwa na serikali ili kukuza uchumi wa taifa na mtu binafsi.

# Hii ndiyo maana halisi ya Pasaka

Na Dk. Enock Mlyuka



Sehemu ya waumini wa dini ya Kikristo wakiwa katika ibada. **PICHA:MAKTABA**

PASAKA ni Sikukuu muhimu sana katika kalenda ya Kikristo na huadhimishwa na maelfu ya watu duaniani. Pamoja na umuhimu wake ukweli huo, watu wengi wanasherehekea Pasaka pasipo kuifahamu vizuri.

Sikukuu ya Pasaka, kiasili, inapatikana katika Agano la Kale la Biblia Takatifu. Neno tunalolisikia mara kwa mara 'Pasaka' linatokana na neno la Kiebrania 'pesach' . Katika lugha ya Kiyunani ni 'to pascha', maana yake kuruka au kupita na katika Kiingereza neno 'passover', maana yake ni 'pita juu'.

Kila familia ya Kiyahudi ilitakiwa kumchukua mwanakondoo wa kiume mwenye umri wa mwaka mmoja, asiye na kasoro na kumchinja jioni ya 14 ya mwezi wa Abibu/Nisani (Machi-Aprili). Sehemu ya damu ya mwanakondoo aliyechinjwa, ilinyunyizwa nje katika milango ya nyumba walizoishi. Malaika wakati wa usiku wa Pasaka, alipoona damu katika nyumba za Wayahudi (Waisraeli) alipita, hakuua wazaliwa wao wa kwanza.

Kwa mantiki hiyo, kwa damu ya mwana-kondoo aliyechinjwa, Wayahudi waliepuka hukumu ya kifo iliyokuwa juu ya wazaliwa wote wa kwanza wa Misri. Hili lilikuwa pigo la mwisho la Mungu ambalo lisingewapa Wamisri fursa nyingine bali kuwaruhusu Waisraeli waondoke Misri ili kutimiza azma ya Mungu ya kukiokoa Kizazi cha Abrahamu, Isaka na Yakobo kutoka utumwani. Kutokana na tendo hilo, Wayahudi walipata fundisho kuwa Mungu ni Mungu wa Wokovu.

Sikukuu ya Pasaka inaelezwa katika Kitabu cha Kutoka 12:1-14, 21-23; 34:25, 26 kwenye Biblia Takatifu. Waisraeli waliagizwa kula Pasaka wakati wa siku ya kuokolewa kutoka utumwani Misri. Pasaka hiyo iliadhimishwa katika kila jamaa, baba wa nyumba akiwa kiongozi - ni kama alifanya kazi ya ukuhani (Kut.12:21).

Waisraeli waliendelea kuadhimisha Pasaka nyumbani mwao katika mwezi wa Abibu/Nisani kwa kutegemea mwandamo wa mwezi. Maadhimisho hayo yalichukua siku saba. Chakula cha jioni maalumu na mkate usiotiwa chachu, divai, mimea na kondoo hutolewa na familia nzima hukusanyika. Waisraeli waliadhimisha Pasaka hata Kabla ya Waamuzi na Wafalme. Waliadhimisha mahali palipoitwa Gilgali kama ilivyoandikwa katika kitabu cha Yoshua 5:10-12.

Baada ya miaka mingi kupita, utaratibu ulibadilika. Iliwapasa kufanyia Pasaka Yerusalemu, mahali pamoja pa kuabudia baada ya hekalu kujengwa. Walifanya hivyo kwa kufuata agizo la Mungu (Kumbukumbu la Torati 16:1-6). Hata sasa Wayahudi wanaadhimisha Pasaka, ingawa kuna mabadiliko machache.

Kwa kuwa hakuna tena hekalu Yerusalemu ambako mwanakondoo anaweza kuchinjwa, sikukuu ya siku hizi ya Kiyahudi iitwayo 'Seder', haiadhimishwi tena kwa mwanakondoo aliyechinjwa. Chakula cha jioni maalumu na mikate isiyotiwa chachu, divai, na mimea hutolewa na familia nzima hukusanyika. Utaratibu wa maadhimisho huongozwa na kiongozi wa familia (baba). Wayahudi hawaadhimishi Pasaka kama tukio la kihistoria tu bali husherehekea uhuru wao pia, siku ya maisha mapya.

### MAANA YA PASAKA KWA WAYAHUDI

Pasaka ilikuwa ya maana sana kwa Wayahudi. Kwa kifupi, Pasaka ilikuwa alama ya uhusiano kati ya Mungu na watu wake na pia alama ya agano. Mungu alisisitiza kuwa yeye ni Mungu wa watu wake na atawaokoa toka utumwani. Pasaka pia ilikuwa alama ya watu wa Mungu. Wale waliokula Pasaka walikuwa watu wa Mungu, ndio aliowachagua kuwa taifa lake takatifu.

Pia Pasaka ni alama ya utii. Kwa Wayahudi, itikio la kufanya Pasaka lilionyesha utii kamili wa agizo la Mungu. Pasaka pia ni kwa kuwa Wayahudi waliamini kuwa Mungu wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo alikuwa Mungu wa kweli.

Ni alama ya kuonyesha kuwapo kwa Mungu. Mungu alikuwa pamoja nao akipita na kuangalia mateso yao na kuwapitia asiwauwe wazaliwa wao wa kwanza. Waliamini kuwa Mungu yuko, anasema, anaagiza, anatuma watu wake na anasikia kilio chao.

Sambamba na hayo, ni alama ya hukumu kwa wasiomcha Mungu. Wamisri hawakuwa waamini wa Mungu bali walifuata miungu yao na uganga. Kwa sababu hiyo Mungu aliwapiga mapigo. Pasaka pia ni alama ya nguvu za Mungu. Miungu ya Wamisri haikupindua maagizo ya Mungu. Mungu alijidhihirisha kuwa Mungu mwenye nguvu. Hakuna kiumbe awaye yote anaweza kushindana naye.

### VILE VILE PASAKA NI:-

• Alama ya mwisho wa mateso. Kabla ya siku ya Pasaka, Wayahudi walikuwa katika maisha ya shida na taabu nyingi kwa miaka mingi. Wengi walizaliwa katika mateso na kufia katika mateso Misri.

i. Alama ya wokovu. Kwa tendo la Pasaka, Wayahudi waliokolewa kutoka katika mateso na kifo hasa kwa wazaliwa wa kwanza. Kwa ajili ya kuokolewa ndiyo sababu Mungu aliwasisitizia sana kuwafundisha Watoto wao maana ya Pasaka (Kutoka 12:26,27). Alama hii ya wokovu haikuwa ya wakati huo tu, bali ililenga hata kwa wokovu wa wakati ujao.

ii. Alama ya mwanzo mpya wa maisha. Kwa teolojia ya Waisraeli Pasaka ilianzisha kitu kipya kabisa. Ni kwamba kila Myahudi alipata maisha mapya, maisha ya uhuru kamili. Wayahudi baada ya kutoka Misri waliendelea kusherehekea siku ya maisha mapya, siku ya uhuru. Katika siku ya uhuru Mungu alijitambulisha kwao kuwa ndiye Mungu wao na Musa atawaongoza. Farao hana tena madaraka juu ya taifa la Israeli.

iii. Ni alama ya kuungwa pamoja. Wayahudi (Waisraeli) waliokuwa wametawanyika kwa kufuata makabila yao 12 sasa waliunganishwa pamoja chini ya Mungu mmoja. Waisraeli walijitambua kwa uwazi zaidi kuwa ni taifa moja, lenye uongozi mmoja na kuabudu kumoja. Wote waliungwa kwa damu ya kondoo. Teolojia ya Agano la Kale inakaza sana kuhusu umuhimu wa damu hasa kama kiungo kati ya Mungu na watu na kati ya watu na mtu.

iv. Alama ya shukrani kwa Mungu kwa tendo la wokovu na uhuru.

v. Alama ya kuwa na matumaini. Waisraeli mioyoni mwao walitoa kondoo wa Pasaka wakiwa na matumaini kuwa wazaliwa wao wa kwanza hawatauawa, hawatakaa Misri tena kwa kuwa ahadi ya Mungu itatimilika-agano alilolitoa kwa Abrahamu, Isaka, na Yakobo kuwa uzao wao utakuwa mwingi na watairithi nchi.

Pasaka ilikuwa ya msingi katika mafundisho ya imani ya Wayahudi katika nyakati za Agano la Kale na inaendelea kuwa msingi katika mafundisho ya imani ya Wayahudi na Wakristo katika nyakati za Agano Jipya.

Katika Agano Jipya, inaelezwa kuwa akiwa na umri wa miaka 12, Yesu alipelekwa na wazazi wake Yerusalemu kula sikukuu ya Pasaka (Luka 2:41-50) na baadaye katika maisha yake, alikuwa na desturi ya kwenda Yerusalemu kula sikukuu ya Pasaka (Yohana.2:13). Chakula cha jioni cha mwisho ambacho Yesu alikula na wanafunzi wake Yerusalemu, mapema kabla ya kusulubiwa msalabani kilikuwa ni Chakula cha Pasaka (Mathato 26:1-2, 17-29). Yesu mwenyewe alisulubiwa siku ya Pasaka ya Kiyahudi (Ijumaa) kama Mwanakondoo wa Pasaka.

### PASAKA KWA WAKRISTO

Maadhimisho ya Pasaka kwa Wakristo ni utimilifu wa ahadi za Agano la Kale na za Yesu Kristo mwenyewe wakati wa maisha yake duniani. Ahadi hizo zinathibitishwa na tendo la kufufuka kwake. Ufufuko wa Yesu ni wa pekee kwani unapita kutoka hali ya kifo na kuingia katika maisha mengine, maisha ya umilele yasiyofungwa na mipaka ya wakati au mahali. Ni maisha yasiyokufa kamwe.

Kama ilivyoelezwa awali, Wayahudi walikombolewa kwa damu ya mnyama (Mwanakondoo), bali Wakristo tumekombolewa kwa mateso na kifo cha Yesu msalabani ili wautoke katika utumwa wa dhambi na mwenendo usiofaa. Wokovu kwa njia ya damu ya Yesu Kristo, hupatikana kwa njia ya utii utokanao na imani (Warumi 1:5;16:26). Yesu Kristo ni pasaka kwa Wakristo, aliyetolewa kuwa sadaka (1Wakorinto 5:7) na ambaye anaishi kwa tendo la ufufuko. Yesu Kristo awaokoa katika nguvu za uovu na kuwaletea ukombozi kwa njia ya msamaha wa dhambi (Wakolosai 1:13).

Kufufuka kwa Yesu Kristo ni msingi wa imani ya Kikristo na kumeongeza thamani ya Ukristo na huduma ya Kanisa. Mtume Paulo anasisitiza akisema, "Kama Kristo naye hakufufuka, basi, kuhubiri kwetu ni bure na imani yenu ni Bure" (1Wakorintho 15:14). Pia kufufuka kwa Yesu Kristo kumeleta tumaini jipya na uhai mpya wa kiroho kwa Wakristo. Kufa na kufufuka kwa Yesu kumewaokoa na mauti ya kiroho (1Wakorintho Kor.10:16-17; 11:24-26) na kwamba, wafu watafufuliwa siku ya mwisho.

Kufufuka kwa Yesu Kristo kumeleta furaha. Wakati wa Pasaka Wakristo wanakumbushwa kutokubeba habari mbaya zenye kuleta mateso, maumivu na kuondoa furaha. Watu wanapaswa kubeba habari zenye kuleta furaha.

Kufufuka kwa Yesu kunawavuta Wakristo katika maisha ya kutokukata tamaa na kutokuishi maisha ya hofu.

Sikukuu ya Pasaka inawakumbusha kuwa Mungu ana uweza. Watu wakipatwa na huzuni, yeye ni furaha yetu. Wakipatwa na matatizo, yeye ni jibu na uponyaji.

Watu wasiangalie tu matatizo na changamoto wanazokutana nazo, bali waangalie ukuu wa Mungu katika maisha. Yeye ni msaada wetu wakati wa mateso. Jambo la msingi ni kuwa watii na kumtumaini.

Pasaka ni Sikukuu ya mabadiliko ya kiroho na si vyakula au mavazi tu. Haipaswi kusherehekewa kwa mazoea, bali watu waruhusu mabadiliko ndani mwao. Iwakumbushe watu kuacha mienendo na tabia mbaya kama vile ulevi, wizi, usaliti, ukatili, fitina, majungu, uongo, mafarakano, uonevu, uvivu, uchoyo, ubinafsi, upendeleo na ulozi. Watu wanakumbushwa kujali na kuthamini watu wengine ikiwa shukrani kwa Mungu.

# Bashe awabana waliokopa wakulima tumbaku

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, ameziagiza halmashauri kushirikiana na wakuu wa mikoa kuzikamata na kuzifikisha mahakamani kampuni zinazodaiwa na wakulima wa zao la tumbaku, fedha zinazofikia Sh. bilioni nne.

Kadhalika, amemwagiza Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, kuhakikisha vyama vinalipa fedha katika mabenki kwa sababu wakulima wameshalipa katika vyama husika.

Waziri Bashe alitoa maagizo hayo jana wakati wa mkutano wa wadau wa tasnia ya tumbaku uliofanyika jana jijini Dodoma.

Alisema ni kosa kubwa kukaa na malipo ya wakulima ndani ya mwaka kitendo ambacho ni kuwarudisha nyuma katika kilimo wanachofanya.

Alisema anahitaji kupata taarifa ya watu kukamatwa na kuchukuliwa hatua ili kulipa madeni ya wakulima.

"Ninaziagiza halmashauri na wakuu wa mikoa hakikisheni kampuni hizo zinakamatwa na kufikishwa mahakamani," aliagiza Bashe.

Alisema wakulima hulima mazao na kupeleka katika kampuni hizo ambazo hukaa na fedha zao kinyume na sheria, hivyo wanapaswa kuchukuliwa hatua.

Bashe alisema hadi kufikia Jumatano, vyama hivyo vinatakiwa viwe vimekutana na kutoa taarifa sahihi kuhusu madai yao katika benki.

Alisema anaamini wakulima wamelipa fedha hizo isipokuwa vyama ndivyo vinavyochelewesha malipo kwa wakulima.

"Kitendo hicho sio kizuri kwa kuwa, wanachelewesha maendeleo ya wakulima, kwa sababu na wao watachelewa kupata uwezeshaji kutoka katika benki.

Mkurugenzi wa Bodi ya Tumbaku, Stanley Mnozya, alisema wakulima wanadai fedha kutoka kwa kampuni, lakini anaamini zitalipwa ili waendelee na kilimo.

Alisema lengo lao ni kuona wakulima wanapata stahiki zao ambazo zitawasaidia kupiga hatua katika kilimo ambacho wanafanya.

Akizungumzia kuhusu kilimo hivyo, alisema msimu ujao wamejipanga kuzalisha tani nyingi ili kuweza kuingia katika ushindani wa uzalishaji zao hilo.

Alisema nchi ya Zimbabwe inaongozwa katika uzalishaji, lakini wanajipanga kuhakikisha wanawafikia ama kuwapita katika uzalishaji wa zao hilo.

Awali, mkulima wa tumbaku, Hamza Rajabu, aliomba serikali kuingilia kati madai yao ili waweze kulipwa stahiki zao wanazodai kutoka katika kampuni.




Vyombo vya usafiri vikipita kwenye dimbwi kubwa la maji ya mvua yaliyotuama katika eneo la Kitunda Kizuani jijini Dar es Salaam juzi kutokana na mvua kubwa ya masika inayoendelea kunyesha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwanafunzi aliyeng'atwa na nyoka na kuzuiwa hospitalini, alipiwa deni

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MWANAFUNZI wa Kidato cha Kwanza katika Shule ya Sekondari Miyandi, wilayani Ikungi, mkoani hapa, Felista Charles (16), aliyezuiwa hospitalini kwa siku saba baada ya kushindwa kulipa deni la Sh. milioni 1.3 ameruhusiwa baada ya Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi kulilipa.

Binti huyo ambaye alilazwa Hospitali Teule ya Makiungu kwa matibabu baada ya kung'atwa na nyoka Machi 21, mwaka huu, aliruhusiwa baada ya afya yake kuimarika lakini kutokana na deni aliendelea kubaki hospitalini hapo.

Mama mzazi wa mwanafunzi huyo, Sisilia Neriko, akizungumza na mwandishi wa habari hizi jana, alisema waliruhusiwa kutoka hospitalini tangu (Machi 21) baada ya hali ya mgonjwa kuimarika, lakini uongozi wa hospitali hiyo uliwazuia kutoka hadi deni la Sh. 1,350,000 lilipwe.

"Tangu tuliporuhusiwa kutoka tumekaa hospitalini siku saba hivyo tumetoka Machi 28, 2024 baada ya fedha kulipwa. Tunawashukuru viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi na uongozi wa Shule ya Sekondari Miyandi kwa kufanikisha suala hili, Mungu awabariki," alisema.

Januari 23, mwaka huu, mwanafunzi huyo aling'atwa na nyoka katika mguu wake wakati akilima katika shamba la moja wa walimu shuleni hapo aliyefahamika kwa jina moja la Robert, baada ya kupewa adhabu ya kufanya kazi shambani humo.

Alisema baada ya tukio hilo, walimu wa shule hiyo walimpeleka kwa mganga wa kienyeji anayefahamika kwa jina maarufu la njoka ambaye inaaminika hutibu wagonjwa waliong'atwa na nyoka, lakini alishindwa kutokana na sumu kusambaa na mguu kuvimba.

Neriko alisema baada ya hali mwanafunzi kuwa mbaya ndipo wazazi walijulishwa ambapo baba mzazi, Charles James, alikwenda kwa mganga huyo wa kienyeji kumchukua kwa pikipiki.

Alisema kutokana na hali ya mtoto kuwa mbaya na kushindwa kukaa katika pikipiki, walilazimika kukodi gari la kumpeleka katika Hospitali Teule ya Makiungu.

Alisema mwanafunzi huyo alifikishwa hospitalini hapo Januari 24, mwaka huu, na siku iliyofuata alifanyiwa upasuaji wa mguu kuondoa baadhi ya nyama kwenye mguu ili kuzuia sumu ya nyoka isiendelee kusambaa mwilini.

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 16214 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE PATRICE YOHANA BUREHE**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY PATRICK STEPHANO MINANI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20th day of April 2024.
Dated at Korogwe this 21st day of March 2024

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 11446 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE RAPHAEL SIMON MDAKI**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY BENJAMINI SIMON MDAKI**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 27th day of March 2024.
Dated at Korogwe this 7th day of February 2024

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI......89......LA 2024**
**FRAZINA GWIMO**
**HERIETH GWIMO**
**MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MEJA GENERAL DENIS JENG**
**MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**
**MEJA GENERAL DENIS JANGA**
**POPOTE ULIPO/MLIPO**
**FRAZINA GWIMO NA MWENZAKE** wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni ( Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 18/4/2024 saa 3:00 Asubuhi/mchana mbele ya Mh J.W.SILLAS Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 28 Mwezi 03/ 2024

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

Ndugu **HASHIMU ABDUL KASIGARA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba **T476BYU.** Taarifa imetolewa kituo cha Polisi Bukoba kwa RB namba **PHQ/KAG/BUK/3225/2024**. Yeyote atakayeiona anaombwa kutoa taarifa kituo chochote cha Polisi

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 16131 OF 2024**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE JOHN MDOE CHANGWA**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY MATRIDA JOHN MDOE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**
ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20th day of April 2024.
Dated at Korogwe this 21st day of March 2024

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO BOMA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**MKOA WA MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi Na...17/2024**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU: LEILA MAULID SUMVYA wa KINGO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA MAULID MTIMA HASSAN**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5 (2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo Tarehe 02 Mwezi 04 Mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Zingatia;

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia

Imetolewa leo tarehe 28 mwezi 03 mwaka 2024

.............................................
**HAKIMU**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Pasaka iwe chachu ili kuleta mabadiliko kwa Watanzania

**LEO** ni Pasaka. Wakristo nchini wanaungana na wenzao duniani kote kukumbuka kufufuka kwa Mwokozi wao, Yesu Kristo, yapata miaka 2,000 iliyopita. Sikukuu hii inaadhimishwa ikiwa ni siku ya tatu, kwa mujibu wa Maandiko Matakatifu, baada ya kuteswa, kuangikwa msalabani na hatimaye kufa na kuzikwa.

Sikukuu hii inasherehekewa baada ya juzi kuadhimisha Ijumaa Kuu, ikiwa ni kumbukumbu ya kuteswa hadi kufa kwa Mwokozi wao, huhanikizwa na ibada mbalimbali katika makanisa na madhehebu mbalimbali, huku maaskofu, wachungaji na mapadri wakitoa ujumbe mbalimbali kupitia mahubiri yao unaohusu maisha ya Ukristo na yale ya kawaida. Pia viongozi wa serikali hutoa salamu na ujumbe katika ibada zile za kitaifa na za kawaida.

Wakristo, hasa wale ambao hufuata imani sawasawa, wanasherehekea Pasaka ikiwa pia ni kumalizika kwa mfungo wa Kwaresma. Waumini hao hufunga siku 40 kama alivyofanya Yesu Kristo na hatimaye akajaribiwa na shetani.

Mbali na Pasaka kuadhimishwa kwa ibada, nchini Tanzania Wakristo huungana pia na watu wa imani zingine katika kusherehekea kwa kula na kunywa kutokana na mizizi ya kihistoria iliyojengwa kuonyesha kuwa wananchi ni wamoja na wanashirikiana katika masuala mbalimbali bila kujali imani, asili, kabila wala itikadi zao. Ndiyo maana licha ya ibada, katika kusherehekea Sikukuu za Kikristo na zile za Kiislamu, watu hujumuika pamoja katika kula na kunywa.

Kama ilivyo ada, baada ya kufanyika kwa ibada, watu watajumuika majumbani na kwenye maeneo ya burudani kwa ajili ya kubadilishana mawazo, kula na kunywa.

Pamoja na kwamba ni sikukuu kubwa kwa Wakristo katika kukumbuka maisha ya Yesu Kristo na kwamba ni ushindi kwao kutokana na kufufuka kwake, baadhi ya watu huigeuza kuwa siku ya kuyageukia mambo ya zamani waliyokuwa wakiyafanya kabla ya Kwaresma.

Katika kipindi cha Kwaresma, baadhi ya watu hufunga na wengine kujizuia kufanya matendo ambayo ni kinyume cha maisha halisi ya Ukristo lakini inapofika siku kama ya leo, huyageukia mambo yale na kufanya maasi. Watu hao hulewa kupitiliza na wengine kuendelea kufanya uasherati na hata ushirikina. Kwa maneno mengine, watu hao hula matapishi yao.

Kwa ujumla, Pasaka ina maana pana kwa maana ni zaidi ya kushangilia kufufuka kwa Yesu Kristo ambaye kwa imani ya Kikristo, Mwenyezi Mungu alimleta duniani kwa ajili ya ukombozi wa wanadamu kutoka katika maisha ya dhambi na kuwapatanisha naye baada ya uasi uliofanywa na Adam na Hawa na hatimaye kufarakana na Mungu.

Kutokana na imani hiyo na kwamba Yesu Kristo amefufuka, hivyo waamini wamepata ushindi, ni vyema watu wakayaendeleza mambo mazuri waliyokuwa wakiyafanya katika kipindi ha mfungo wa Kwaresma kwa kutenda mema na kujizuia kutenda baadhi ya mambo ambayo ni chukizo mbele za Mungu. Wakristo hawana budi kuamini kwamba kwa kufa na kufufuka kwake, ameshinda dhambi na wako huru dhidi ya mambo yote ambayo hufanywa katika giza na uovu.

Mwanafalsafa na Kiongozi wa zamani wa India, Mahatma Gandhi, aliwahi kusema: "Iwapo Wakristo wangeishi maisha kama aliyoyaishi Yesu Kristo, dunia ingekuwa na amani." Lakini kutokana na watu hao na wengine duniani kuishi maisha yaliyo kinyume na Yesu Kristo, dunia imejaa machafuko, maasi na mabaya ya kila aina, hivyo amani na upendano vimetoweka.


Hayo yote yamesababisha kuwapo kwa mapigano baina ya taifa na taifa, kabila na kabila, watu kukosa hofu ya Mungu, wenye nacho kuwanyanyasa wasio nacho, walioko madarakani kutumia nafasi zao kujinufaisha badala ya kuwajali wananchi.

Wakati leo Wakristo duniani kote wanaadhimisha siku hii ya kipekee ya Pasaka, wanapaswa kurejea misingi ya imani hiyo kwa kuyaacha mambo yasiyo faa na kutenda mambo na kuishi maisha kama aliyoyaishi Yesu Kristo alipokuwa duniani.

Ni imani kwamba waumini hao kama watafanya mambo yenye ushuhuda mwema na kujiepusha na tamaa na kufanya yaliyo chukizo mbele za Mwenyezi Mungu na wanadamu, hakika kutakuwa na mabadiliko chanya na Tanzania itakuwa kielelezo cha watu Afrika na dunia nzima.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Bodaboda wadhibitiwe wasizidi kusababisha ajali zisizo za lazima

**TAASISI** ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu (MOI) inaeleza kuwa hupokea majeruhi wa ajali za bodaboda wastani wa watu tisa hadi 10 kwa siku.

Mwaka jana, Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Respicious Boniface alikaririwa na vyombo vya habari akisema, kuna ongezeko la ajali za bodaboda kwa kutofuatwa kwa sheria ya usalama barabarani.

Katika hilo, anasema waathirika wengi hawavai kofia ngumu (Helment), na kwamba kuna ongezeko la ajali kwa asilimia tano hadi sita kwa mwaka, huku kwa siku wakipokea majeruhi wa ajali za barabarani 10 hadi 15 kati ya hao 10 wakiwa ni bodaboda.

Aidha, katika maelezo yake, anasema, kwa mwezi wanapokea majeruhi 350 hadi 400 huku wa bodaboda wakiwa 280, kitendo kinachoonyesha kuwa kuna wingi wa ajali za bodaboda.

Nimejaribu kufafanua kidogo kile ambacho kimeelezwa na mtaalam wa afya, na sasa ni vyema nijikite kwenye hoja kwamba, kuwapo kwa fursa ya kuendesha pikipiki za kubeba abiria (bodaboda), kumewaondoa baadhi ya vijana vijiweni wanachakarika kutengeneza maisha.

Pamoja na kuwapo kwa fursa hiyo, ni vyema wangezingatia sheria ya usalama barabarani kwa ajili ya usalama wao na wa abiria badala kuendesha vyombo hivyo vya moto kienyeji.

Mtindo wa kuendesha bodaboda bila kuvaa kofia ngumu, kuvuka kwenye makutano ya barabara bila kuruhusiwa na taa za kuongozea vyombo vya moto na makosa mengine mengi yanawakabili wao.

Imekuwa kawaida kwao kukuta gari limesimama kwenye eneo la pundamilia au kwenye makutano ya barabara kusubiri waenda kwa miguu wapite au kusubiri taa ziruhusu, lakini wanapita bila kujali.

kuna haja sasa kwa askari wa usalama barabarani, kuelekeza nguvu kwa madereva hao ili kuwapusha na ajali zinazotokana na uzembe wao unasababisha abiria kujeruhiwa au kupoteza maisha.

Inashangaza na inasikitisha kuona muda wote wao wana haraka, na wanakosa umakini wawapo barabarani na wanabaki wakivizia kupenya hata katika maeneo ambayo ni ya hatari kwao.

Kama inawezekana, askari wa usalama barabarani wangebuni mbinu ambazo zingesaidia kuwafanya wafuate sheria bila shuruti ili wanapofika kwenye eneo la pundamilia au kwenye mataa, wasimame.

Inawezekana mtindo wao huo wa kutofuata sheria, walishagonga waenda kwa miguu au kupata ajali ambayo inasababisha hata wenyewe na abiria wao kujeruhiwa au kupoteza maisha.

Miaka ya nyuma, madereva hao walituhumiwa kwa wizi, katika maeneo mbalimbali ya jijiji la Dar es Salaam, kwamba wanapora mikoba ya watu wanaokutana nao barabarani kutokomea kusikojulikana.

Mbali na hilo walituhumiwa pia kwa kupora bodaboda za wenzao, lakini sasa tatizo ambalo ni kama limeota mizizi, ni la kutofuata sheria ya usalama barabarani ambalo ninadhani linawasababishia ajali.

Kama ni mafunzo na semina, wamekuwa wakipewa mara kwa mara ili wazingatie sheria lakini baadhi yao wamekuwa ni wagumu hadi washurutishwe, hivyo, ningekuwa ni vyema kama askari wataelekeza nguvu katika kuwadhibiti wale wasiozingatia sheria.

Imekuwa kawaida askari wa usalama barabarani kusimama kando ya makutano ya barabara ili kuongoza madereva wa vyombo vya moto, lakini madereva wa bodaboda hupenya bila kuruhusiwa.

Katika mazingira hayo, askari nao huwa wanawaacha, aidha kwa kuona kuwa wameshindikana, au kwa namna yoyote ile. Lakini ninadhani ipo haja ya kuwachukulia hatua zaidi madereva wa aina hiyo.

Wanaona ni jambo la kawaida kutotii sheria, matokeo yake ni wanasababishia wengine ajali. Ni vyema wabanwe zaidi ili watii sheria badala ya kufanya wanavyotaka kana kwamba hakuna wa kuwadhibiti.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Pasaka ina maana zaidi kwa Wakristo



Pascal Mayalla

Leo ni Jumapili ya Pasaka. Hii ndiyo siku aliyoifanya Bwana tuishangilie na tuifurahie. Ni siku ya ufufuko wa Bwana Yesu Kristo. Ni siku ya tatu baada ya kifo chake. Kwa Wayahudi ni siku ya kwanza ya juma. Hii ni kwa sababu siku za Kiyahudi zilianza jioni na kuisha jioni.

JUMAPILI ya leo ni Sikukuu ya Pasaka, hivyo naomba nianze makala yangu kwa kuwatakia Wakristo na Watanzania wote Heri ya Pasaka.

Dini kuu mbili za Tanzania, Wakristo na Waislamu, zote zina sikukuu mbili mbili kubwa. Kwa Waislamu ni Sikukuu ya Iddi El Fitri na Sikukuu ya Iddi El Haj. Shamrashamra za kusherehekea Idi el Fitri na kubwa na inasherehekewa na watu wa dini zote mbili pamoja na kuvaa nguo mpya kwa watoto.

Kwa Wakristo, sikukuu mbili ni Krisimasi na Pasaka. Krismasi ni kusherehekea kuzaliwa kwa Masiha, Yesu Kristo na Pasaka ni kusheherekea kufufuka kwake. Krisimasi ndiyo yenye maandalizi ya muda mrefu na husheherekewa kwa shamrashamra sana kuliko Pasaka. lakini ukweli ni kwamba Pasaka ndiyo sikukuu yenye maana kubwa kwa Wakristo kuliko Krismasi kutokana na kitu kinachoitwa Fumbo la Pasaka ambalo ndilo kiini cha Imani ya Ukristo.

Fumbo la Imani ya Ukristo ni kuamini Kristo alikufa, alifufuka na atakuja tena. Kristo kabla ya kufa, alisulubiwa kwa ajili ya Wakristo, akateswa kwa mamlaka ya Pontio Pilato, akafa, akazikwa.

Akafufuka siku ya tatu kama ilivyoandikwa katika maandiko matakatifu.

Fumbo la Pasaka ni kiini cha imani ya Kanisa inayopaswa kutangazwa na kushuhudiwa kwa watu wa mataifa. Kwa njia ya mateso, kifo, ufufuko kutoka kwa wafu na kupaa mbinguni, mwanadamu amekombolewa kutoka katika dhambi na mauti.

Leo ni Jumapili ya Pasaka. Hii ndiyo siku aliyoifanya Bwana tuishangilie na tuifurahie. Ni siku ya ufufuko wa Bwana Yesu Kristo. Ni siku ya tatu baada ya kifo chake. Kwa Wayahudi ni siku ya kwanza ya juma. Hii ni kwa sababu siku za Kiyahudi zilianza jioni na kuisha jioni.

Wayahudi hawakuhesabu siku kwa kuanzia saa sita ya usiku hadi saa sita ya usiku kama nyakati zetu. Ilipofika saa ya machweo yaani jua lilipoanza kuzama, siku iliisha na mara siku mpya ilianza.

Yesu alizikwa siku ya Ijumaa, akashinda siku nzima, siku ya Jumamosi hadi mapambazuko ya siku ya Jumapili. Hizo ni siku tatu. Tunazihesabu tatu, si kadiri ya masaa 24 bali kadiri ya majina ya siku jinsi walivyohesabu Wayahudi.

Kwa nini tarehe ya kuadhimisha Pasaka hubadilika kila mwaka? Sikuu ya Pasaka ya Wayahudi iliitwa 'Passover'.

Ili kuepuka Pasaka kuangukia siku za katikati ya juma, ni lazima iadhimishwe siku ya Jumapili ambayo ni siku ya kwanza ya juma, yaani Jumapili.

Kwa mantiki hiyo, Jumapili ni siku ya kwanza ya juma, siku ya ufufuko. Ni siku ya uumbaji mpya tunaporudishiwa sura na mfano wa Mungu tulioupoteza kwa dhambi ya asili. Pasaka ni sikukuu Kuu. Pasaka ya sasa si tena ile Pasaka ya Wayahudi, waliyokumbuka kutolewa kwao utumwani Misri bali ni siku ya kukombolewa kutoka utumwa wa dhambi na nguvu za shetani.

**UFUFUKO WA YESU**

Kwa desturi ya Wayahudi, mwili wa mtu aliyekufa akazikwa, alipaswa kupakwa mafuta kwa siku tatu baada ya kuzikwa kwa sababu waliamini kwamba roho ya mtu aliyekufa hubaki karibu na mwili kwa siku tatu na siku ya nne huenda kwa Mungu.

Kwa sababu hiyo, walipaswa kuupaka mafuta mwili wa Yesu kwa siku tatu. Yesu alikufa siku ya Ijumaa, hivyo alipaswa kupakwa mafuta mara ya kwanza kabla ya kuzikwa. Siku iliyofuata ilikuwa sabato pia ilikuwa sikukuu kubwa ya Pasaka ya Wayahudi, hivyo hawakumpaka Yesu mafuta. Hii ni kwa sababu siku hiyo hawakuruhusiwa kufanya kazi yeyote.

Baada ya sabato ilifuata Jumapili, siku ya kwanza ya juma ambayo ndiyo siku ya tatu baada ya Yesu kufa.

Wanawake walikwenda kuupaka mwili wa Yesu mafuta mapema asubuhi. Walikuta kaburi liko wazi na Yesu amekwishafufuka, sasa ni mzima. Hili ndilo fumbo la Pasaka.

Ufufuko wa Yesu Kristo ndio msingi wa imani Ukristo. Kuteswa kwake kwa kupigwa mijeledi, kuvikwa taji la miiba, kutemewa mate, kutundikwa msalabani, kufa na kuzikwa kisha kufufuka, ndicho hasa kilele cha fumbo la ukombozi wa Ukristo.

**WANAWAKE WATU MUHIMU KWA MUNGU**

Kuna kasumba ya kuwadharau wanawake katika dini kuu zote mbili kwa kutoruhusiwa kuwa Maimamu na makasisi katika Kanisa Katoliki. Lakini kwa Mungu, wanawake ni watu muhimu.

Ni Wanawake ndio waliokwenda alfajiri kaburini kuupaka mwili wake mafuta na ndio wanashuhudia kuwa Yesu Kristo amefufuka na baada ya kufufuka aliwatokea kwanza wanawake. Hiyo ni kuonyesha umuhimu wa wanawake.

Ufufuko ni mabadiliko kutoka utu wa kale kwenda utu upya, kutoka maisha ya dhambi kwenda maisha ya utakatifu.

Ufufuko wa Yesu Kristo ni wokovu wa Ukristo kwa kukombolewa kutoka mautini na kuwekwa huru kutoka utumwa wa shetani na upotevu wa milele. Mlango wa paradiso uliofungwa kutokana na dhambi ya asili ya Adamu na Eva, au Adamu na Hawa, umefunguliwa kwa kifo na ufufuko wa mwana wa Adamu, yaani Yesu Kristo.

Pasaka ni Habari Njema kwa Wakristo kwamba Kristo Mfufuka yuko kati yao, yuko pamoja nao na ndani ya kila mmoja wao. Kristo ameshinda dhambi na kifo,

**Heri ya Pasaka**
**Paskali**
**0754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Kwani Watanzania wakiambiwa ukweli wana shida?



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

HII Tanzania yetu ukikaa na kuifikiria, wakati mwingine unaona kama mwisho wa dunia unakaribia, kwa jinsi mambo yanavyokwenda, hasa masuala ya kisiasa yanavyokuwa yanashika kasi mpaka kufikia mengine kuficha uhalifu.

Unakaa unasikia huyu analalamikia hili na yule analia na la kwake, lakini wanaoliliwa hujitokeza na kujibu nusunusu ilimradi wakijua hata ukipiga kelele hakuna linalofanyika kuondoa malalamiko na vilio vyako vya kila siku na kila mara.

Mathalan, siku za karibuni kuna wanasiasa waliibuka na kilio cha wabunge kulipwa mishahara ya Sh. milioni 18 kwa mwezi, tena wakisema hiyo ni nyongeza ya Sh milioni tano kwani awali walikuwa wakilipwa Sh. milioni 13.

Katika kulisakafia hilo, wakasema walianza kulipwa hivyo kipindi kile cha malumbano ya mwekezaji wetu kipenzi wa bandari ya Dar es Salaam, jamaa zetu maarufu wa Dipii Welidi ambao tayari wameshaanza mambo yao katika bandari hiyo.

Eti waliongezwa ili kuhakikisha Dipii anakubaliwa kuwekeza katika bandari hiyo na ndicho kilichotokea. Hivi sasa magati kadhaa ni yake na sasa wanaambiwa wafanyakazi kuchagua kubaki Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari au kwenda Dipii.

Lakini Bunge kwa upande wake, likaona kama linachafuliwa na wasaka hulua Ikulu, kwa kutamka uongo mchana kweupe na kukanusha kuwa si kweli. Limesema hakuna mbunge analipwa kiasi hicho cha fedha kwa mwezi. Likaulizwa basi wanalipwa kiasi gani? Likasema mshahara wa mtu ni siri!

Sisi mashabiki wa siasa, yaani wananchi wapigakura, ambao ndio tunaokamuliwa ili kulipa mishahara hiyo, tukabaki hatujui ni kiasi gani wanalipwa ila kuamini tu kuwa wanalipwa Sh. milioni 18 kwa mwezi kwa sababu hatujaambiwa kiasi kingine zaidi ya hicho!

Wakati tafrani hiyo ikiendelea, likaibuka lingine la kisiasa pia. Hili likihusisha gari 'Vieite' lililokamatwa Manyara likiwa na wahamiaji haramu 20 kutoka Ethiopia, likiendeshwa na Edward Erihard.

Kisiasa, gari hilo lilikuwa likipeperusha bendera ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), hivyo sisi kina 'pangu pakavu tia mchuzi' tukasema ni la CCM na linafanya hivyo kwa maslahi ya CCM au mwana CCM.

Mara moja Mwenezi wa CCM wa Mkoa wa Manyara, John Nzwalile, akaibuka na kulikana huku akilaani waliotumia bendera hiyo kwenye livieite hilo, lenye uwezo wa kubeba abiria saba tu, kwa maslahi yao binafsi.

Hata kama si la CCM hivi kweli wahamiaji haramu kutoka Arusha kuja kukamatwa Manyara, ina maana humo njiani hakukuwa na mtu aliyewasimamisha mpaka kukamatwa kwenye kituo cha Minjingu, Babati kweli?

Ingawa CCM ilikanusha kuwa gari hilo haliwahusu, lilitumia tu bendera na msimamo huo ukaungwa mkono na Idara ya Uhamiaji Manyara bila hata kujishughulisha kufanya kiuchunguzi cha kina, hakuna aliyesema nani mmiliki halali wa gari hilo.

Hivi wangejipa muda mfupi kuulizia hata Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kujua umiliki halali wa gari hilo wangepoteza nini mpaka kuibuka na kusema halina uhusiano kabisa kabisa na CCM? Je, kama mmiliki ni kada wa CCM linakosa uhusiano kabisa kabisa kweli?

Nafikiria tu kuwa endapo jivieite hilo namba T 774 BDL lingekuwa linamilikiwa na Mwenyekiti tuseme wa chama cha upinzani katika kata moja tuseme ya Ilala au Mjumbe wa Baraza Kuu la Wazazi la chama pinzani, hivi ingekuwaje?

Ni imani yangu angeanikwa hadharani na kuwekwa mahali pasipo salama kutokana na kusafirisha wahamiaji haramu na asingesubiriwa mpaka afike Minjingu ndipo akamatwe. Mpinzani? Thubutu!

Maana yake ni kwamba mtindo wa kupeperusha bendera hizo za CCM kwenye magari au maeneo mbalimbali huwa ni njia ya kuficha uhalifu kwani inajulikana njiani magari yenye namba za serikali, mashirika au taasisi za umma na chama tawala, yana uhalali usio rasmi wa kufanya yatakavyo.

Magari au wamiliki wao huonekana kana kwamba wako juu ya sheria na kuwakamata ni kosa la jinai, hivyo kuachwa wakisigina sheria za barabarani wanavyotaka, ilimradi maslahi yao kwanza.

Mara ngapi hata jijini Dar es Salaam, licha ya polisi kukataza magari yasiyo mabasi yaendayo haraka, kupita kwenye njia zao lakini ndio kwanza ya serikali na CCM yanaongoza kupita humo yakipishana na 'maofisa usafirishaji' wetu-madereva bodaboda!

Ili kuwatendea haki Watanzania, Bunge liseme wabunge wanapokea mishahara kiasi gani.

Lakini pia hilo jivieite tuambiwe ni la nani na tuelezwe kwa nini linashiriki uovu kwa kusafirisha wahamiaji haramu? Jenerali Jacob Mkunda upo? Kazi Iendelee!

## Shule 113 zapewa vitabu mtaala mpya

**Na Steven William,** MUHEZA

HALMASHAIRI ya Wilaya ya Muheza, Mkoani Tanga, kupitia Idara ya Elimu Msingi imepokea vitabu 16,104 aina mbalimbali vya Mtaala Mpya Ulioboreshwa na kuvigawa katika shule za msingi 113 za serikali kwa lengo la kuboresha mazingira ya elimu.

Ofisa Elimu Vifaa na Takwimu wa Wilaya hiyo, Flora Kahana, alikabadhi vitabu hivyo juzi katika hafla fupi iliyofanyika katika Kata ya Nkumba.

Flora alisema vitabu hivyo ni vya madarasa ya awali hadi darasa la tatu, ikiwa ni jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan, katika kuboresha mazingira ya kupata elimu na kuongeza viwango elimu.

Mratibu wa Elimu Kata ya Nkumba, wilayani Muheza, Athumani Msamba, alimshukuru Rais Samia kwa juhudi za kuwapatia vitabu ambavyo vinakwenda kurahisisha mazingira ya kufundishia.

## TARURA yajenga daraja lililokatika

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) imekamilisha ujenzi wa daraja linalounganisha kata za Minyughe na Makilawa, Ikungi mkoani Singida lililokatika miaka mitatu iliyopita kwa gharama ya Sh. bilioni 1.6. Mtendaji Mkuu wa TARURA, Mhandisi Victor Seff, alisema juzi kuwa kukatika kwa daraja hilo kuliathiri shughuli za kiuchumi na upatikanaji wa huduma za kijamii ikiwemo afya na elimu.

Alisema kukamilika kwa daraja hilo la chuma lenye urefu wa mita 30 katika barabara ya Mtamaa-Minyughe hadi Mtavira, wilayani Ikungi, litafungua fursa ya kiuchumi kwa wananchi wa kata hizo.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Singida, Mhandisi Ibrahim Kibasa, alisema kukamilisha uunganishaji wa vyuma kwa ajili ya daraja hilo, kumewezesha mto Minyughe kufunguka na hivyo kutoa fursa kwa shughuli za uchukuzi kuendelea kati ya maeneo ya vijijini na makao makuu ya mkoa.

Alisema kwa sasa wananchi wa kata tatu zinazounganishwa na daraja hilo, wataweza kuzikabili changamoto mbalimbali zilizokwamisha shughuli zao hususani wakati wa masika kutokana na mto kufurika maji kiasi cha kutishia usalama wao wakati wa kuvuka.

"Sehemu ya fedha hizo ni bajeti ya mwaka huu ambapo tumejenga madaraja ikiwemo daraja hili la Minyughe, daraja hili limekuwa likiwasumbua wananchi takribani miaka mitatu na hivyo kukwamisha utekelezaji wa shughuli za kiuchumi kwa wananchi wa Kata tatu pamoja na Mkoa wa jirani wa Tabora, katika wilaya ya Uyui, inayopakana na wilaya hii ya Ikungi,"alisema.

Aidha, Mhandisi Kibasa alisema, ujenzi wa daraja hilo umetokana na bajeti ya mwaka iliyotengwa kiasi cha Sh. bilioni 4.4 katika Wilaya ya Ikungi kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya barabara na madaraja katika halmashauri ya Wilaya hiyo.

Baadhi ya wananchi walioshuhudia kukamilika kwa kazi hiyo, akiwamo Bi. Elizabeth Bakari wa Kijiji cha Minyughe na diwani wa Kata Minyughe , Nelson Kiwesi, waliishukuru Serikali kwa mradi huo ambao baada ya kukamilika unakwenda kuondoa adha ya usafiri hasa kwa wajawazito.

# Kampeni nishati safi kupikia yashika kasi

**Na Beatrice Shayo**

WAKATI serikali ikiendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, Kampuni ya Taifa Gas Tanzania Limited imesema imejipanga kufikisha huduma ya gesi nchi nzima kwa gharama nafuu ili wananchi wasiendelee kupata madhara katika afya zao.

Meneja Mauzo wa Taifa Gas, Joseph Nzumbi, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari katika hafla ya futari waliyoiandaa kwa watu mbalimbali.

Alisema Taifa Gas imeweka mikakati ya kupambana na ukataji wa miti unaoendelea kwa sasa, kwa kuendelea kutoa elimu ya matumizi ya nishati safi.

"Tunawapa watu elimu kwa njia mbalimbali kuhusu matumizi ya gesi lakini pia tunashirikiana na sekta mbalimbali katika kuendeleza kampeni ya matumizi ya nishati safi na hivi karibuni tumetoa mitungi 10,000 ili kuhamasisha watu watoke kwenye matumizi ya nishati chafu na waingie kwenye matumizi ya nishati safi," alisema.

Alisema wamekuwa na kikundi kinaitwa 'Wanawake na Samia' ambapo wamewapatia elimu ya matumizi ya gesi na kuwapa duka ambalo watakuwa wanalisimamia na kuuza ili kujipatia kipato lengo ni watu waweze kuwa na uelewa.

"Bei tulizoziweka kwenye soko ni nafuu, sisi kama Taifa Gas malengo yetu kufikisha huduma ya gesi kote nchini ili wananchi watumie nishati safi kwa kupika kwa gharama ndogo," alisema.

Aidha, alisema matumizi ya gesi ni rahisi ukilinganisha na matumizi ya mkaa ambayo ina gharama kubwa na unaweza kupata madhara kwa afya ya binadamu.

"Ukiangalia mtu anayetumia mkaa na gesi kiujumla mimi ninamuona anayetumia mkaa ni tajiri zaidi kwani anayetumia mkaa kwa mwezi atatumia120,000 kwa mtu mwenye familia ya watu watano, lakini ukiwa na Taifa Gas utatumia sh 55,000 kwa mtungi wa kilo 15," alisema.

Naye Meneja Biashara wa kampuni hiyo, Bhoke Angellah, alisema takwimu zinaonesha kuwa, takribani watu 33,000 wanapoteza maisha kwa mwaka kutokana na matumizi ya mkaa na kuni jambo ambalo ni hatari kwa wananchi.

"Watu hawa wanaopoteza maisha wengi wao ni wanawake sababu mara nyingi wanakuwa jikoni. Kwa hiyo sisi kama Taifa Gas tumelitambua hilo na ndio maana tumeweka mikakati ya kutosha juhudi zetu nyingi tunaziweka kwa kinamama ambao wao kwa namna moja au nyingine wanafanya maamuzi kuhusu nishati ipi anaitumia akiwa jikoni.

"Kwa hiyo kina mama wana jukumu kuhakikisha anatumia nishati safi na kuna dhana kuwa chakula kinachopikiwa gas sio kizuri hususani wali, hii sio kweli hiyo dhana tuiondoe na waandishi wa habari tunaomba mtusaidiane kuelimisha jamii kuhusiana na hili, watu elfu 33 ni wengi kuwapoteza," alisema.

Pia alisema kuna dhana potofu ya baadhi kudai ukipika chakula kwenye gesi kinapoteza ladha jambo ambalo si kweli.



Eneo la barabara ya vumbi likiwa limeharibika vibaya Kitunda kwenda Magole jijini Dar es Salaam kutokana na mvua inayoendelea kunyesha. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mzee wa kanisa afuturisha Waislamu

**Na Steven William,** MUHEZA

MZEE wa Kanisa la Waadventista Wasabato la Muheza Central, wilayani hapa mkoani Tanga, John Mdoe, amewafuturisha waumini wa dini ya Kiislamu.

Mdoe kwa kushirikiana na familia yake, wametoa sadaka hiyo kwa zaidi ya Waislamu 100 juzi nyumbani kwake, Mtaa wa Mdote. Mgeni rasmi alikuwa Shekhe wa Wilaya ya Muheza, Abdallah Seif na ilihudhuriwa pia na Katibu wa BAKWATA Wilaya hiyo, Shabani Nguzo.

Viongozi hao wa dini walitumia hafla hiyo pia kuiombea nchi amani, utulivu na mshikamano pamoja na kuombea viongozi wa taifa wakiongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Mdoe alitumia fursa hiyo pia kukabidhi zawadi ya nguo aina ya kanga na cheti cha Ramadhani Kareem kwa Shekhe wa Wilaya Seif na Katibu wa BAKWATA wilaya, Nguzo.

Akizungumza wakati wa futari hiyo, mzee huyo alisema Kanisa la Waadventista Wasabato linaamini kuhusu uhusiano mzuri baina ya Wasabato na dini ya Kiislamu.

Mchungaji wa Kanisa la Sabato, Mtaa wa Michungwani Muheza Mjini, Daud Masindi, alisema katika kipindi hiki cha mfungo wa Ramadhani, hiyo iwe ni sehemu ya kusema hao ni ndugu zao. "Iwe sehemu ya kuungana nanyi kumwomba Mwenyezi Mungu ili aweze kutupa amani katika maisha yetu, jamii zetu, taifa letu la Tanzania. Tunamwomba Mungu amjaalie Rais Samia na viongozi serikalini amani," alisema.

Shekhe wa Wilaya ya Muheza, Abdallah Seif, alimpongeza na kumshukuru Mzee wa Kanisa hilo kwa kuandaa futari hiyo na kusisitiza kuwa, ni jambo la kheri na la kuigwa ambalo linaleta umoja na amani kwa nchi.

Katibu wa BAKWATA wa Wilaya, Nguzo, alisema wataendelea kutoa ushirikiano kwa wakristo katika wilaya hiyo ili kudumisha upendo, umoja na mshikamano.

# MAISHA

MACHI 31, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14

**CHAPATI ZA NDIZI**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**

Ishi nyumba inayokupa furaha, amani



Ukurasa 13

**MITINDO**



# JAZA NYWELE KIASILI

Ukurasa 14

## WATOTO


### MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| U | | T | A | I | F | A |
| S | | | | M | | N |
| H | | F | A | A | | D |
| I | B | A | | R | A | I |
| N | | N | O | A | | K |
| D | | Y | | | | I |
| I | D | A | K | E | | A |


### FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

DUA, NIA, WAO, RAI, IBARA, SHINA, DONDA, IMARA, UDIWANI, ANZISHA

### TOA TOFAUTI 5




### PAKA RANGI




### AMSHA AKILI




### CHEKA



Alichokifanya daktari

Msikie mtoto huyu akimuuliza maswali baba yake.

**Mtoto:** Baba unaweza kumwachia hilo gari lako dada wa kazi akaliendesha?

**Baba:** Siwezi kumwachia gari langu hili aliendeshe ni ghali sana.

**Mtoto:** Je, mnaweza kumwachia chumba chenu dada wa kazi kikiwa wazi na mkaenda kazini?

**Baba:** Haiwezekani kamwe, kuna vitu vya gharama na pia heshima haitakuwepo.

**Mtoto:** unaweza ukampa dada kadi ya ATM yako na namba ya siri ukachukulie pesa?

**Baba:** Mtoto una balaa wewe, unataka siku akiiba hii kadi akachukue pesa zote tuwe maskini, sithubutu.

**Mtoto:** aahaaaaaa, kumbe hauwezi kumkabidhi chochote chenye thamani dada wa kazi, sasa kwa nini mnanikabidhi mimi kwake nyie mnaenda kazini mpaka mnarudi, kumbe mimi sina thamani kwenu eeeeh

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kulikoni kasi wake kukimbia waume zao?

KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze duru letu la Maisha Ndivyo Yalivyo. Bado jicho letu liko kwenye ndoa. Wiki iliyopita nilisema maisha ya ndoa ni safari ndefu. Kuna wakati mtafurahi na nyakati zitawalazimu kulia.

Kuna wakati mtapishana katika uamuzi na wakati maisha ya uchumi wenu yanaweza kushuka. Hapa ndipo kuvumiliana na kutiana moyo kunahitajika sana.

Aidha, kuna wakati mnaweza kugongana mawazo na wakati mmoja wenu anaweza kuugua. Hapo ndipo upendo wa kujitoa unatakiwa kudhihirika kwa kila mmoja. Ndoa hii itaweza kusimama tu pale wana ndoa watakapokuwa na upendo wa Mungu kwa kushikamana.

Pamoja na ukweli huo, bado wanandoa wengi wamekuwa hawana uvumilivu inapotokea sintofahamu katika maisha yao ya ndoa. Matokeo yake mawazo mbadala huchipuka na kugawanyika, hatimaye kusambaratika.

Msomaji wangu, nikumegee visa viwili vinavyoonyesha ndoa zilizoparaganyika, kisa mwanamume kapigwa kiuchumi. Maisha yalianza vizuri ndiyo maana hata ndoa kufungwa lakini baada ya muda, hali ikawa si hali na matokeo yake ndoa kubomoka.

> **“Mke wangu kashanikimbia kitambo. Nikiahidiwa kazi inaahirishwa. Nina ujuzi wa kazi saba lakini kula yangu tu ni shida. Kiufupi nina nuksi hatari! Naombeni msaada ndugu zangu mnisaidie”**

Wako vijana wawili nilizungumza nao, mmoja wao kupitia ujumbe wa simu ya kiganjani, wakielezea ugumu wa maisha na yale wanayopitia hadi kujikuta wakikimbiwa na wake zao na kubaki njia panda wasijue cha kufanya.

Kijana mmoja aitwaye James (27), mkazi wa Ifaraka mkoani Morogoro, nikiwa natoka kanisani, nilimkuta na mwenzake wakiwa wameketi karibu na gereji ya bajaji. Nikawapatia kipeperushi kuwaalika kwenye kongamano la maombi.

Baada ya kuwashuhudia, nikataka kujua kwa nini wako pale. Ndipo James akafungaka na kueleza yale anapitia. Akasema: “Hapa na rafiki yangu huyu tumezunguka huko na huko kubahatisha kazi lakini hatujafanikiwa. Mimi ni mchoraji wa mabango na kadhalika.

“Wakati mwingine sipati kazi nakosa hela ya kula. Nimeoa na nina mtoto mmoja. Mke wangu baada ya kuona maisha magumu, alivizia sipo akachukua vitu vyote pamoja na kompyuta mbili za kufanyia kazi akatoroka na mtoto kwenda kwao Dodoma.

“Hapa nilipo sina vifaa vya kazi aliondoka navyo. Natamani nipate nauli niende kwetu Ifakara nikauze sehemu ya shamba langu ninunue kompyuta nyingine niendelee na uchoraji na utengenezaji wa mabango.”

Mpenzi msomaji, huyo ndiye James akitafakari maisha. Mkewe kama angekuwa na upendo wa dhati, angejadiliana na mwenzake kuhusu kwenda kwao.

Pia asingechukua vifaa vya kazi ili mumewe aendelee kujiimarisha kiuchumi.

Shida mwanamke hakuwa mvumilivu. Hata hivyo, nilimsaidia kijana huyu nauli akaondoka kwenda Ifakara ambako bado anatafuta mnunuzi wa shamba lake apate mtaji wa kujiendeleza kimaisha.

Kijana mwingine anaitwa Mussa wa huko Chunya mkoani Mbeya. Huyu alinitumia ujumbe mfupi kwenye simu ya kiganjani. Akasema: “Naitwa Mussa nina umri wa miaka 32 nipo hapa Chunya! Naomba msaada wa kiroho popote ulipo. Usiku naota nafanya kazi, nikiamka nimechoka sana. Kila kazi ninayofanya inakufa.

“Mke wangu kashanikimbia kitambo. Nikiahidiwa kazi inaahirishwa. Nina ujuzi wa kazi saba lakini kula yangu tu ni shida. Kiufupi nina nuksi hatari! Naombeni msaada ndugu zangu mnisaidie”, anamaliza ujumbe wake.

Mpenzi msomaji, bila shaka umepata picha kwa yale wanayopitia vijana hawa wawili. Tatizo kubwa sana ambalo mwanadamu anaweza kupitia katika maisha yake ni tatizo la ndoa. Ni rahisi kukabiliana na changamoto ya biashara lakini si rahisi kukabiliana na mafarakano katika ndoa.

Mungu ameshaweka bayana kwenye moja ya maandiko yake kwamba “mwanamke ni mlinzi wa mume”. Ni “msaidizi”, Mungu alipomuumba mwanadamu wa kwanza, Adamu, alimpatia mwanamke, Hawa, kuwa msaidizi wake kumuondolea upweke.

Hii ina maana kwamba pale mwanaume anapooa halafu mwanamke akaondoka, maisha hupwaya kwani hana msaidizi wala ulinzi. Shetani ndiye kinara wa kumshawishi mwanamke ili atengane na mume wake.

Ndiyo maana tunaweza kuona kwamba matatizo makubwa katika ndoa za watu wengi yana chimbuko refu sana la ki-shetani. Wengi wanaopitia matatizo makubwa ya ndoa hawajui kuwa nguvu za giza zimeachiliwa kuua hatma za maisha yao.

Mwanamke badala ya kuikimbia ndoa, yampasa kupiga magoti kumsihi Mungu aingilie kati kuokoa ndoa hiyo. Bila shaka msomaji umejifunza jambo hapo.

**Je, una maoni, kisa, ushauri? Ujumbe 0715268581. Na hii pia ipo WhatsApp.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Ni watoto wa mama au janga kwa taifa?

IDADI ya vijana wa mwendokasi waliooa na wasiomudu kuhudumia familia, huku wakitegemea matunzo, chakula na kuishi kwa baba au mama, sasa ni janga jipya katika taifa letu.

Kwa uchache, taswira ya jumla ya paji la uso la baadhi ya vijana hawa ukiwatazama inazungumza mengi. Ombwe hili sasa litufikirishe kama taifa tunakwenda wapi, tunajinasuaje!

Ni janga linaloashiria taifa limepatwa. Kiza kimeathiri uoni wa wanasiasa wetu hawajajipanga.

Nani aliyeanza kusonya, akionyesha kuumizwa nacho? Wako wanaopuuza na wengine hawaoni kabisa ni tatizo, wanajilamba.

Sasa hivi ukipita kwenye baadhi ya kaya, kuna wimbi kubwa la vijana wenye umri kuanzia miaka 25 mpaka 45 na kuendelea, ambao ni kina ‘kula kacheze’

Kula kacheze, kule kwetu kijijini Sanya Juu, ni vijana wa kiume, ambao wakiamka asubuhi wanakwenda mtaani kucheza korokoro (michezo ya kubahatisha), kamari au kushinda baa na kurudi kula na kulala kwa wazazi wao.

Jamii inaoana ni mzigo kwenye familia lakini msingi wa tatizo hawajui ulianzia kwao. Malezi yao yaligeuzwa na mwiko.

Hilo kundi la mwendokasi, ndoto yao kubwa ni kulelewa. Halina moja, wala mbili. Linawaza bata, kuchanja (kula miraa-mirungi), kula shisha, bangi na pombe.

Kama si Israel nani na aseme sasa? Askofu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Fredrick Shoo, anasema taifa linatishiwa na ongezeko la vijana legelege waliooa lakini bado wanaishi nyumbani kwa baba zao wakiwa tegemezi.

Amekwenda mbali zaidi akisema kanisa linashuhudia wimbi kubwa la wanaume kuteswa, kupigwa na kunyanyaswa na wenzi wao. Kwa minajili hiyo, kanisa limeamua kuhamasisha kuanzishwa kwa kile alichokiita ‘Umoja wa Wanaume’

Askofu Dk.Shoo amenukuliwa akisema umoja huo wa wanaume unatafakarisha na kutoa somo kwao kwa kuwa sasa mambo yamebadilika na wao wanahitaji kufarijiana na kusaidiana.

Katika msingi wa hoja yake, Askofu Dk. Shoo ansema hivi: “Vijana wamekuwa legelege, kijana ameoa lakini bado anakaa kwa baba, anakula kwa baba. Wanaume mashujaa tunapaswa kusimama kama mashujaa wenye maadili ili watoto wetu waige.”

Katika kitabu cha Ujamaa kilichondikwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere Julai, 1968, kimeeleza kuhusu azimio la kukubali aina fulani ya maisha.

> **Sasa hivi ukipita kwenye baadhi ya kaya, kuna wimbi kubwa la vijana wenye umri kuanzia miaka 25 mpaka 45 na kuendelea, ambao ni kina ‘kula kacheze’**

Mwalimu Nyerere amesema: “Katika hali yetu ya sasa ya uchumi na katika umaskini wetu, azimio la kukubali aina fulani ya maisha, linaweza kuonekana kama jambo la vitabuni tu. Lakini ukweli ni kwamba, kuna baadhi ya vitendo ambavyo tutakataa kufanya au kuvikubali kila mtu binafsi au taifa zima, hata kama matokeo ya vitendo hivyo vingeleta ongezeko la uchumi na kutafsiri maendeleo kwa kukua.”

My friend! Hakuna mtu atakayekuja kwenye maisha yako kukutimizia malengo yako, isipokuwa wewe mwenyewe!

Muda unatosha kabisa kutimiza malengo yako, lakini hautoshi kufanya kila kitu kwenye maisha yako.

Kanuni mojawapo ya mafanikio, ambayo unapaswa kuizingatia kama unataka kutoboa katika maisha haya ya sasa, ni kuchukua uamuzi mgumu wa kubadili mwenendo wa maisha yako na malengo yako.

# HARUSI







Ni kumbukumbu nzuri kwa Elisha Mgendi na Adelina Kiondo, wakati walipofunga ndoa Aprili 25 mwaka jana katika Kanisa la Wasabato la mkoani Morogoro.



# MITINDO

## CHOMEKEA UKIPATA FUTARI

WAKATI huu wa mwezi wa Ramadhani, unapata mialiko kadhaa ya kupata futari kutoka sehemu mbalimbali ambazo ni muhimu kwako.

Hata hivyo, unashindwa kuhudhuria kutokana tu huna vazi zuri la kwenda nalo kuhudhuria mlo huo. Kuna njia rahisi ya kukufanya ujumuike na wenzako kula futari kwa furaha, nayo ni kuvaa shati la kuchomekea.

Mtindo huu wa uvaaji humfanya mtu kuwa nadhifu zaidi na mwenye muonekano usiochosha kwa watu wengine.

Jambo la muhimu hapa ni kuchagua suruali nzuri yenye rangi nyeusi au bluu na shati lenye uangavu. Unaweza kuchagua shati jeupe au wenye mchanganyiko wa weupe na rangi zingine kama njano, nyeusi au nyekundu.

**MASHARTI MUHIMU**

Unapotaka kuvaa shati la kuchomekea, ni lazima kuchagua lenye ukubwa sawa na mwili, ukivaa kubwa sana hautapendeza.

Kutokana na uvaaji wa kuchomekea unatumika na watu wastaarabu, epuka kuvaa mlegezo kwani hautakupa taswira nzuri

Jambo lingine muhimu, unapovaa shati na kuchomekea hakikisha fulana ya ndani maarufu kama singlet haionekani kabisa.

Katika kujiweka vizuri zaidi, hakikisha huvai mkanda mrefu au wenye upana unaochosha.

Chini vaa kiatu cha ngozi kinachong'aa. Usivae viatu vya wazi aina ya makubanzi au sando.





URFEMBO

**Na Mary Geofrey**

# JAZA NYWELE KIASILI



NYWELE ni moja ya kiungo kinachoongeza urembo kwa wanawake kwa kumpa muonekano mzuri zaidi.

Katika hitaji la kila mtu, anataka kuwa na nywele nzuri, ndefu na zenye afya.

Lakini kuna baadhi wana nywele ambazo zina tatizo la kudumaa na chache kichwani.

Wenye tatizo hilo wana fursa kujifunza namna ya kutumia matunda na asali kwa ajili ya kurefusha nywele zako.

Kwa kutumia njia hiyo utakuwa na uhakika wa kuwa na nywele ndefu zisizokatika na zilizojaa kichwani.

JINSI YA KUFANYA

Chukua parachichi kubwa moja, asali vijiko vitatu na kiini cha yai.

Osha nywele zako kwa shampoo na kisha uzikaushe.

Ponda ponda parachichi mpaka lilainike kabisa. Chukua vijiko vitatu vya asali na kiini cha yai kisha changanya yote kwa pamoja.

Paka mchanganyiko huo kaa nao kwa muda wa dakika 15 kisha osha.

Fanya hivyo kwa muda wa wiki moja hadi mbili na utaweza kuona matokeo mazuri katika nywele yako.



MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Chapati za mtindi





CHAPATI zilizotengenezwa kwa maziwa ya mtindi ni nzuri kutokana na kuwa laini na zenye protini nyingi.

Chakula hiki kinafaa kuliwa siyo tu kwa kifungua kinywa nyakati za asubuhi, bali huliwa jioni kama mlo kamili.

**MAHITAJI**

Kikombe kimoja na nusu cha chai cha unga wa ngano vya unga wa ngano, sukari vijiko vitatu vya sukari, kijiko kimoja cha baking soda.

Mahitaji mengine ni robo kikombe cha chumvi, maziwa mtindi kikombe kimoja na robo tatu, yai moja, vijiko viwli vya chakula vya siagi, vijiko viwili vya chai vya Vanila na mafuta ya kupikia kadiri ya mahitaji yako.

**NAMNA YA KUPIKA**

Chukua bakuli kubwa, weka unga wa ngano, sukari, baking powder, baking soda na chumvi, kisha changanya vizuri.

Chukua bakuli nyingine ndogo, weka maziwa ya mgando, yai, siagi na vanila, kisha changanya kwa kupiga piga, hadi uone mchanganyiko huo umechanganyika vizuri.

Mimina mchanganyiko huo wa maziwa ya mgando, yai, siagi na vanila kwenye bakuli kubwa lenye mchanganyiko wa ung wa ngano, sukari, baking poda na chumvi.

Kisha changanya kwa kupiga piga na hadi uone mchanganyiko huo umekamilika vizuri.

Weka kikaango kwenye jiko lenye moto wa wastani. Weka kijiko kimoja cha chai cha mafuta ya kupikia kwenye kikaango, kisha yasambaze vizuri.

Mimina robo kikombe cha uji wa chapati kwenye kikaango na usambaze vizuri uji huo kwa kutumia kijiko.

Kaanga upande huo wa kwanza wa chapati kwa muda wa dakika tatu, au hadi utakapo ona upande huo umeiva na kuwa na rangi ya kahawia, halafu geuza upande wa pili kwa muda wa dakika moja au zaidi.

Utakapoona upande huo umeiva na kuwa na rangi ya kahawia, itoe na uiweke kwenye sahani tayari kwa kuliwa.

MAISHA NI NYUMBA

Na Restuta James

## Badili mwonekano kwa 'wall paper'

'WALL PAPER' ni pambo linaloweza kubadili mazingira ya nyumba kwa kiwango kikubwa mno kutokana na aina ya picha zinazotengenezwa kupata aina hiyo ya pambo.

Mwaka 2024 umeanza kwa aina mpya ya wall paper ikiwamo picha inayoonesha jua likizama, ambayo ukiiweka ndani unapata mandhari nzuri.

Iko picha nyingine ya fukwe ikionesha kujaa kwa maji ambayo inaleta mazingira ya utulivu wa hali ya juu.

Mandhari nyingine inayobamba kwenye aina hii ya pambo ni picha ya msitu au bustani ya maua mazuri. Pia picha inayoonesha barabara au mbuga ya wanyama.

Mtaalamu wa mapambo ya nyumbani, Brigitte Didas, anasema picha inayoonesha jua likizama inafaa ile ambayo imepigwa kwa kuchukua mazingira ya mto au maji na aina kiasi ya miti.

Anasema nyingine ni inayoonesha zaidi mawingu na hasa iliyopigwa kwa juu na mtu akiwa ndani ya ndege.

Kwa mujibu wa Brigitte, picha ya msitu inawafaa watu wanaopenda mazingira asilia na kwamba ili ikae vizuri, iwekwe mwishoni mwa korido.

"Wall paper ya hifadhi za wanyama inafaa iwe na kundi la ina moja ya wanyama kama twiga au simba kulingana na mtu anavyopenda, uzuri wa wallpaper ni kwamba ni rahisi kuitoa pale unapohitaji kufanya hivyo wakati wowote," anasema.

Anashauri kuweka aina hizi za wallpaper kwenye ukuta mdogo na hasa kwenye kona ili kuongeza ukubwa wa eneo. Pia ni picha nzuri inayoweza kuwekwa upande wa pili wa kioo.







# Ishi nyumba inayokupa furaha, amani

Habari ndugu wasomaji na wapenzi wa safu hii. Ni matumaini yangu kwamba mko salama, wazima na mna furaha kedekede katika kusherehekea Sikukuu ya Pasaka. Nawatakia wasomaji wangu Heri ya Pasaka.

Kwa kuwa leo ni Sikukuu ya Pasaka, siku ya furaha na amani, basi moja ya mambo ambayo mtu anapaswa kuwa nayo ni maeneo ambayo huwa ya faraja na ya kupumzisha akili baada ya shughuli nyingi ni nyumbani.

Nyumbani ndipo palipo na mkusanyiko wa maisha, kumbukumbu na upendo kwa asilimia kubwa ya watu. Unaweza kukosa amani na furaha mahali popote lakini nyumbani ni lazima kuwe na mazingira ya kukupa furaha.

Binadamu kila mmoja hujishughulisha na mambo mbalimbali lengo likiwa ni kujitafutia riziki na kuhakikisha mkono unakwenda kinywani na mambo mengine ya kimaisha na kifamilia yanakwenda sawa.

Pamoja na kujishughulisha huko, mwisho wa siku lazima arejee nyumbani kujipumzisha bila kujali umbali wake. Kwa hiyo kwa vyovyote vile lazima uhakikishe nyumbani kunakuwa mahali sahihi, panapokupa furaha, amani na utulivu.

Si tu kwa utulivu, ni muhimu kuzingatia kwamba nyumba hiyo ya kuishi iko eneo ambalo halitakusababishia karaha, kuanzia aina ya watu wanaokuzunguka, mandhari yake, ufikikaji wake na vitu vingine muhimu. Utulivu huo si tu kwako, bali na kwa familia yako kwa wale wenye nazo.

Watu wengi hasa tunaopanga, huwa tunakosa utulivu tunapotafuta nyumba kutokana na kutokujipa muda wa kutosha kutafuta nyumba hizo na hivyo wakati mwingine tunajikuta katika wakati mgumu baada ya kuhamia kwenye nyumba ambazo baadae hubaini kwamba aidha hazikuendana na sisi au nyumba zinaendana nasi lakini mazingira yanayozunguka nyumba si rafiki.

Kwa sababu hiyo, watu wengine hulazimika au kutamani kuhama kwenye nyumba ndani ya muda mfupi hata kama pesa ya pango waliyolipia haijaisha.


Moja ya vitu vinavyosababisha watu watamani kuhama kwenye nyumba kabla ya wakati ni pamoja na aina ya majirani wanaowazunguka kwamba baadhi yao ni wakorofi mpaka kufikia hali ya mtu kukosa amani na utulivu. Kila siku migogoro haiishi na watu wanaanzisha jipya kila wakati.

Hata mwenye nyumba mwenyewe anaweza kuwa chanzo cha wewe kutamani kuhama nyumba yake kwa sababu ya 'chokochoko'zake za hapa na pale. Unaweza kuhamia katika nyumba hiyo lakini ukabaini kwamba eneo ilipo nyumba kunafanyika mambo ambayo yako kinyume na wewe au na imani yako, kwa hiyo ikakukosesha amani.

Kutokufanikiwa kutimiza ndoto ya kuishi kwenye nyumba zilizo katika mazingira yanayoendana nasi kunasababisha hata ufanisi katika utendaji kazi wakati mwingine kupungua.

Wakati wote mtu anawaza atakumbana na lipi lingine jipya au kutokuwa na uhakika na amani ya familia yake. Kwa hiyo ni muhimu kuishi kwenye nyumba zilizo katika mazingira yanayoendana na sisi.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
'CHEO'
"HEEEE?!
MTEJA ,MUADILIFU KAMA MIMI NINAYETUMIA MPAKA LAKI TATU PAPO KWA PAPO SIKU NIKIWA SINA KITU?
ATUKOPESHI
KAUNTA
TULIKUCHAGUA UKIWA MWEMBAMBAAAAAAA! NASHANGAA KERO KIBAO UNANENEPEANA!
THATHA KERO THI'DHAKWENU MIE NAKONDAJE?
AKKA! MWANAKWETU ETI' OOH! ANAUBAKA USUKANI...HAMNA HATA HAYA? MSINISIMANGE
DALADALA
SHEREHEKEENI SIKUKUU NA MKIPATACHO NA SIO MKITAKACHO... MABUCHA YAONENI KAMA MAPAMBO
'HOVYO!'
MWENYE MKEWE HAJASAFIRI KWENDA POPOTE NA ROHO BADO INAMUUMA
ILIPATA KIDONDA AU MICHUBUKO?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...SAFU HII INAWATAKIA PASAKA NJEMA MASHABIKI WAKE WOTE...

HABARI KIMATAIFA

# Kunusurika kifo kwa Zuma, ANC yanyooshewa kidole



RAIS wa zamani wa Afrika Kusini Jacob Zuma (pichani), amenusurika katika ajali ya gari usiku wa kuamkia juzi.

Hata hivyo, viongozi wa chama kipya cha Umkhonto We Sizwe (MK) wamekishutumu chama tawala cha ANC kwa kuhusika katika tukio hilo.

Zuma alinusurika kifo baada ya gari lake kugongwa na gari nyingine lililokuwa likiendeshwa na mwanaume mwenye miaka 51, katika jimbo la Kwazulu Natal.

Tukio hilo lilitokea saa chache baada ya maofisa wa tume ya uchaguzi kumzuia Zuma kushiriki katika uchaguzi mkuu utakaofanyika Mei 29, mwaka huu.

Kiongozi huyo na walinzi wake walinusurika katika ajali hiyo ambayo inadaiwa ilisababishwa na dereva aliyekuwa amelewa pombe.

Jeshi la polisi nchini Afrika Kusini lilisema gari la Zuma liligongwa na mwanaume huyo ambaye amekamatwa kwa makosa ya kuendesha gari akiwa amelewa na uzembe barabarani.

Msemaji wa chama MK, Nhlamulo Ndhlela, alisema katika taarifa yake kuwa katika kipindi cha mwaka mmoja na nusu, Zuma amenusurika katika ajali mbili zinazowahusisha madereva wanaodaiwa kuwa walevi.

Ndhlela alisisitiza kuwa inaonekana tukio hilo kama jaribio la makusudi la kutaka kumuua Zuma mwenye umri wa miaka 81, ambaye aliongoza nchi hiyo na mwenye ushawishi nchini humo.

Msemaji huyo aliongeza kuwa chama hicho kimekuwa kikifuatilia kwa karibu mlolongo wa matukio yanayoshabihiana ambayo yamemtokea Zuma chini ya utawala wa serikali ya Cyril Ramaphosa.

Alisema matukio hayo yalianza Desemba mwaka jana baada ya Zuma kutangaza atafanya kampeni kwa tiketi ya chama cha MK.

Binti yake Zuma, Duduzile Zuma, aliandika kwenye ukurasa wa mtandao wake wa kijamii wa X akidai kuwa ajali hiyo ya gari haikuwa bahati mbaya.

"Tafadhali msituone wajinga, sisi sio wafuasi wa Ramaphosa", aliandika Duduzile.

Ndhlela, alibainisha kile alichokiita kauli za hatari zilizotolewa na wanasiasa wa ANC dhidi ya Zuma, na kutolea mfano kauli ya kiongozi mmoja wa mkoa aliyesema kuwa Zuma atakuwa hospitalini kabla ya uchaguzi.

Wakati uchaguzi unakaribia, chama tawala nchini Afrika Kusini cha ANC, kwa mara ya kwanza tangu kilipoingia madarakani 1994, kiko katika hatari ya kupata kura zaidi ya asilimia 50.

Chama hicho kimekuwa kikipoteza uungwaji mkono kutokana na matatizo ya kiuchumi, tuhuma za ufisadi na ubadhirifu wa mali ya umma.

Zuma alihukumiwa kifungo cha miezi 15 jela mnamo Juni, 2021 baada ya kukataa kutoa ushahidi kwa jopo lililokuwa likichunguza kuhusu vitendo vya ufisadi.

Hata hivyo, aliachiliwa huru miezi miwili baada ya kutumikia adhabu kutokana na matatizo ya kiafya.

**DW**



Wakimbizi waliokimbia vita nchini Sudan wakiwa katika kambi ya muda katika eneo la Zam Zam nje ya mji wa El-Fashir , Darfur jana.
**PICHA: AP**

## Israel yakubali mazungumzo

**TEL AVIV,** ISRAEL

SERIKALI ya Israel imekubali kuendelea na mazungumzo ambayo yanakaribia kufikia makubaliano ya kusitisha vita na kuwaachia mateka ambao bado wanashikiliwa na kundi la wanamgambo la Hamas.

Ofisi ya Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyau, ilisema kwamba, wajumbe wa ngazi ya juu watasafiri kuelekea Qatar na Misri ndani ya siku zijazo kuendelea na mazungumzo.

Kulingana na taarifa hiyo, Netanyahu alitoa hakikisho kwamba timu yake ya majadiliano inayoongozwa na mkuu wa idara ya ujasusi ya nje Mossad na ile ya ujasusi wa ndani Shin Bet, watakuwa na fursa ya ushawishi katika mazungumzo hayo.

Nchi za Marekani, Qatar na Misri zimekuwa zikifanya upatanishi baina ya Israel na Hamas kwa wiki kadhaa ili kufikia mwafaka wa kusitisha vita Gaza na kubadilishana mateka na wafungwa.

Hata hivyo, kikwazo kilikuwa kwa Netanyau ambaye alionekana kuwa na msimamo mkali wa kuendeleza mapigano, jambo ambalo lilionekana kuudhi Marekani ambayo ni mshirika wake mkubwa.

**DW**

# Mbabe wa Haiti atoa sharti kumaliza ghasia

**PORT-AU-PRINCE,** HAITI

MMOJA wa viongozi wa magenge wenye nguvu nchini Haiti, amesema atafikiria kuweka chini silaha ikiwa watashirikishwa katika mazungumzo ya kuanzisha serikali mpya.

Vikundi vinavyoongozwa na Jimmy Chérizier, anayejulikana kama Barbecue, vinadhibiti sehemu kubwa ya mji mkuu wa nhi hiyo Port-au-Prince.

Cherizier alitabiri ghasia ndani ya taifa hilo masikini zitaongezeka katika siku zijazo.

Aliiambia shirika la habari la Sky News la Uingereza kwamba wako tayari kwa kutafuta suluhu.

Taifa hilo lenye watu zaidi ya milioni 11, limekuwa bila waziri mkuu tangu Machi 12, mwaka huu.

Waziri Mkuu Ariel Henry, alijiuzulu baada ya kuzuiwa na magenge yenye silaha kurejea nchini kwake baada ya kutoka Kenya, ambako alikwenda kutia saini mkataba wa kupelekwa kikosi cha kulinda amani.

Baraza la Mpito la Rais lilianzishwa ili kuandaa mpango wa kurudisha utawala wa kidemokrasia ambao unaungwa nkono na Marekani.

Cherizier, ambaye ni mashuhuri zaidi katika muungano wa magenge ya kihalifu unaojulikana kama Viv Ansanm , alisema kundi lake linafaa kuwa na kiti katika meza ya mazungumzo.

"Ikiwa jumuiya ya kimataifa itakuja na mpango wa kina ambapo tunaweza kuketi pamoja na kuzungumza, lakini hawalazimishi kile tunachopaswa kuamua, nadhani kwamba silaha zinaweza kupunguzwa." alisema Cherizier.

Alisema hajisikii fahari kuona ghasia zinazoendelea nchini humo na alionya kwamba mgogoro unaweza kuendelea ikiwa makundi kama yake, ambayo yanapinga wanasiasa wafisadi hawata kuwa sehemu ya serikali.

Aidha, alisema vikosi vyovyote vya Kenya vilivyoandaliwa kuingia nchini humo ili kuimarisha usalama vitachukuliwa kuwa wavamizi.

**BBC**

MAKALA

# HUU NI UDUMAVU WA AKILI



Na Magabilo Masambu

> **Kuna hoja za baadhi ya watu kutumiwa kutokana na hali zao za kimaumbile na kimaisha kutajirisha baadhi ya watu mijini. Kwamba, unamkuta mtu ni ombaomba lakini anahifadhiwa na mtu fulani na ndiye anayemtumia kuomba ili kila inapofika jioni wanagawana mapato.**

CONNECTION' ni neno lenye maana ya kiunganishi, lakini limekuwa maarufu sana katika siku za hivi karibuni, huku likitamkwa kwa Kiswahili na kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Siku za hivi karibuni kama si zamani sana dhana ya kiunganishi au kuunganishiwa mambo imekuwa kubwa sana katika jamii yetu na dhana hii sasa imegeuka na kuwa kama tabia mpya inayopendwa kutumiwa zaidi na vijana hasa wale waliomaliza na wanaomaliza masomo katika taasisi mbalimbali za kati na za juu.

Naweza kuiita dhana hii kama ugonjwa unaosababisha hali ya ulemavu na udumavu katika akili za watu wengi, kiasi cha kushindwa kufanya shughuli au mambo yao kwa kuamini kwamba ili kupata au kufanya shughuli zao, wanahitaji watu wengine kuwasaidia ama kupata au kufanya kazi hizo.

Binafsi, ninakubali kwamba yako mazingira yanahitaji msaada wa mtu mwingine ili kufika mahali fulani. Lakini kwa sasa hata zile shughuli ambazo tungeliweza kuzifanya wenyewe, hatufanyi na badala yake tunangoja 'connection' ili kuzifanya.

Wazazi zetu wengi walipata maisha mazuri kwa kuyahangaikia sana huku leo wakitaka tutumie njia zile zile ili tuyapate maisha yale yale waliyoyatafuta kwa shida. Kinyume chake tunawaona kuwa ni wakoloni. Tumetaka sana mtelezo, mambo yatokee kirahisi rahisi na kwamba dunia ya sasa si kama ya zamani lakini ubaya wa kuyapata maisha kirahisi, lazima tujue kwamba pia yataondoka kirahisi.

Iko hadithi ya mtu mmoja katika Biblia. Mtu huyu aliugua kwa muda mrefu karibu miaka 38 na Yesu alipomwona alimwuliza: "Wataka kuwa mzima?" Yule mtu akamwambia: "Bwana mimi sina mtu wa kunitia birikani maji yanapotibuliwa, kila wakati ninapokuja mimi, mtu mwingine hushuka mbele yangu."

Ni kweli kwamba mwenye hali mbaya anahitaji kutiwa birikani ili kupona, lakini utamaduni huu mpya unawajumuisha hata wasio na hali mbaya kujiona kwamba wanahitaji 'connection'.

Hali ya kuamini kwamba ili ufike mahali fulani unahitaji kushikwa mkono, imezuia ubinifu na stadi za vijana wengi. Badala yake kila mmoja anangoja apelekwe anapopataka. Utaratibu huu unafanya watu kufanya kazi wasizozihitaji na matokeo yake ni kuharibu kazi huku wakilipwa mishahara kwa sababu si kazi wanazozipenda.

Hawazifanyi kwa moyo na wenye mioyo na kazi hizo kwa sababu hawana wa kuwaweka birikani. Wamebaki wamelala chini kama yule mgonjwa.

Iko dhana pia kwamba mali nyingi zinazoachwa na wale wamiliki wa kwanza wanapofariki dunia, baada ya muda mfupi, mali nazo zinaisha. Ni matokeo ya kuwaachia watu ambao walizoea kushikwa mkono badala ya kuwa na juhudi binafsi.

Mtoto anaanza darasa la kwanza mpaka anamaliza chuo kikuu hakuna mahali amewahi kufanya kibarua au kazi kwa kutafuta mwenyewe. Kila kitu anamtanguliza baba, mama, mjomba na kadhalika. Mwenyewe hawezi kwenda kwa msimamizi wa kazi na kumwambia nimekuja naomba kibarua au kazi badala yake anataka apewe memo na baba yake kwamba nenda kamwone fulani. Katika hili, nasema kutoka katika sakafu ya moyo wangu kwamba tunajenga taifa la ovyo sana.

Haya mambo yanaanza mbali. Unakuta mtoto yuko kidato cha pili hawezi kufua nguo zake. Mkimaliza kula chakula, hawezi kufuta meza na kunawisha watu. Naye ni bwana mkubwa, hawezi kuosha hata vyombo. Mwisho wa siku, hata kujitegemea kiakili pia inakuwa taabu.

Hii imesababisha kwa sasa kila anayemaliza chuo kikuu, haamini kupata kazi kwa kutafuta mwenyewe. Anaamini wanaopata wote wamesaidiwa na pia waliyofanikiwa wamesaidiwa mtu.

Kama huyu anaweza kuwa na jembe ndani, shamba analo na mvua iinanyesha na bado analalama kwamba ana njaa nyumbani kwa sababu hana mtu wa kumsaidia na asiposaidiwa anajenga uhasama, inashangaza sana na huu ni udumavu wa akili. Maisha yako unalaumu watu kwa kushindwa kukusaidia?. Ooo! Mimi nina mjomba jeshini ameshindwa kunisaidia niingie huku. Inaingia akilini?

Katika kuhangaika kwangu, nimegundua kwamba wako baadhi ya mabosi katika ofisi hawataki memo ndipo wakusaidie ukienda kwa sababu inakuwa kama amri. Baadhi wangefurahi kukuona mhusika mwenyewe badala ya kwenda na kikaratasi au nimetumwa na fulani. Tusiogope ofisi hizi ni zetu, hakuna mtu atakupiga ukimwambia nimekuja kutafuta kazi.

Kwa ushauri wangu, ukitaka kufanikiwa kwa mengi, ondoa fikra za kusaidiwa maana ni fikra tegemezi na hakuna umasikini mbaya kama kuwa na mawazo tegemezi. Tafsiri yake ni kwamba, hakuna siku utachukua hatua ya kufanya jambo. Kila kitu unataka kusaidiwa au kuuliza wakati uwezo unao, nguvu na akili ya kufanya hayo unavyo.

Jiamini wewe mwenyewe kwani unaweza kuacha kutegemea watu kwani Waswahili wana msemo kwamba mtegemea cha nduguye hufa masikini. Inawezekana wakati unakwenda kusoma chuo kikuu ulijua mjomba ni Kamanda wa Polisi wa Mkoa (RPC) unakuja kumaliza masomo mjomba ameshafariki dunia. Lazima utapoteza mwelekeo. Mjomba awapo au asiwepo, jenga utamaduni wa kuamini unaweza kufanya mwenyewe.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**Dar es salaam-Tanzania**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Ndiyo nashindia uji, kweli navaa mitumba, lakini hayo hayakuhusu*



Na Adam Fungamwango

> **Asubuhi shuleni, jioni tuisheni, usiku vyumbani. Na siku za sikukuu au mapumziko watakuwa wanacheza ndani ya ukuta wao. Kama wanasoma shule moja watajuana lakini si vinginevyo. Kila mmoja kashika lake.**

MADA hii waliozaliwa na kulelewa 'uzunguni' hawataielewa kivile. Wengine watabaki wanashangaa.

Watoto kama wa Masaki, Oysterbay, Upanga, Mbezi Beach, Dar es Salaam na mikoa mingine ambayo ina sehemu zinazoitwa 'uzunguni', wakisoma baadhi wataishia kucheka na kuona kumbe kuna aina fulani ya maisha ambayo hawajawahi kupitia.

Wale wenzangu na mimi walizaliwa na kukulia uswahilini, wenyewe wanaita 'uswazi', hata kama hivi sasa wanaishi 'uzunguni', wataelewa na kukumbuka mbali sana. Maisha yana mapito mengi.

Maeneo kama Mburahati, Kigogo, Tandale, Mabibo, Mwananyamala, Kinondoni, Magomeni, Mbagala, Tandika, Temeke, Dar es Salaam huko ndiko uswazi sasa.

Hata kwenye mikoa mingine nchini yapo maeneo mengi ambayo jamii imejikusanya na kuishi kwa pamoja, kama vile nyumba za kota, na mengine yanayofanana na hivyo.

Maisha ya 'uzunguni' ni kwamba kila nyumba ina geti, na imezungshiwa ukuta, hivyo kila familia inakuwa kivyake. Hakuna mambo ya kuamka na kuanza kusalimiana asubuhi mmeamkaje, wala mmeshindaje.

Wanaopakana wanaweza kuishi hata miezi na miezi wasionane. Wanaweza kuonana kwa bahati mbaya, kila mmoja akiwa anatoka getini au kuingia na gari lake. Au shida yoyote kubwa na ya kimsingi na si kuombana chumvi, sukari wala kibiriti.

Ni mara chache sana kuona watoto wao wakicheza pamoja. Asubuhi shuleni, jioni tuisheni, usiku vyumbani. Na siku za sikukuu au mapumziko watakuwa wanacheza ndani ya ukuta wao. Kama wanasoma shule moja watajuana lakini si vinginevyo. Kila mmoja kashika lake.

Huku uswahilini maisha hawako hivyo. Unaweza ukaamka asubuhi ukagongewa mlango wakati una usingizi bado, halafu aliyekugongea nia yake ni kukusalimia tu kujua kama umemka salama.

Na huko kama huna tabia ya kusamilia watu, kuongea nao, au kujumuika kwenye shughuli, matatizo, au misiba, basi utatengwa. Kikikupata cha kukupata hakuna yoyote atakayefika kwako.

Maisha ya pande zote mbili yana faida na hasara zake. Pamoja na faida nyingi za watu waliokulia uswahilini, lakini kwenye mada hii nitazitaja hasara zake.

Moja kati ya hasara kubwa ni kufuatiliana maisha. Kuna watu huko wao kazi yao moja tu. Akiamka anataka kujua fulani kama nini, amevaa vipi, amefanya nini na akijua yeye ni kusambaza kwa wengine.

Hawa watu huwa hawalipwi, ila kwao wanaona fahari sana kufanya kazi hiyo. Hawa wanaitwa wambea. Hii tabia ni kama kilema tu. Mtu huyu anaweza kupoteza muda wake na gharama kwenda kupeleka habari za mtu kwa wengine hata kama wakataa mbali, ili mradi tu wanafahamiana.

Wengine ni wafitini, wagombanishi, na wana roho mbaya. Ukila vizuri anachukia. Haendi kusema kwa majirani. Ila ukila vibaya yeye anafurahi. Atakwenda kutangaza kitu ulichokula. Lakini jana ulikula vizuri hakutangaza. Akawa amenuna.

Tulioishi uswahilini tunajua vizuri habari hizo. Unaweza kununiwa wiki nzima kwa kunywa chai ya maziwa tu. Au wiki mzima umefululiza wali usiku. Utaona mama yako ananuniwa na kutengwa kwa muda. Ila siku mkinywa chai ya rangi, mchana ugali dagaa, usiku ugali, kesho wanarudisha urafiki, lakini na kutetwa juu.

Ndiyo maana mwanamuziki Marijani Rajabu, akatunga kibao kimoja kinachoitwa 'Ubaya wa Jirani', ambao stori yake ni hiyo hiyo ya mambo yanayotendeka uswazi.

"Nyota njema imewaka aa, mambo yangu yamenyooka aa, maisha yamebadilika, baada ya dhiki faraja. Lakini bado nashangazwa, jirani yangu kaka sirika, hata jambo hataki kunipa, sijui nilichomkosa.

Anacheka jino pembee eeehe, moyoni anasononeka, kwa nini huyu yuko vile nami niko hivi, moyo wamuuma.

"Alitaka niwe duni, hata nisiwe na thamani, lakini jitihada zake na matakwa yake havishindi kudura. Anasahau hata Mungu baba, kwamba yeye ndiyo mtoaji, jirani angepewa jungu la kugawa ridhiki, ingekuwa vipi. Pilipili asoila hahahaha, yeye inamuwashia nini, kupata kwangu au kukosa simzidishii wala simpunguzii

"Nyota njema imewaka aa, mambo yangu yamenyooka aa, maisha yamebadilika, baada ya dhiki faraja. Kunichunguza ati nakula nini. Kunichunguza ati leo navaa vipi. Kuvaa na kula kwangu wakutakia nini.

Hata kama niliwa navaa kaniki, hata kama nilivaa suti ya pande tatu, haya yote jirani hayakuhusu wee.

"Hata nikishindia uji wa chenga, hata nikila biriani kwa kuku, haya yote jirani hayakuhusu wee. Nilipokuwa sina kitu hata hukunijali. Na kazi unayoifanya wala hukuithamini. Ulisema mimi bure nahangaika, wala hakuna chochote kinachopata."

Huku ndiko 'uswazi' bwana. Wale wa Oysterbay hebu mtuache kwanza.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba aliyomwelekeza aende kumuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, saa chache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-1

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ALICHOAMUA ni kuchukua sufuria la ugali alilosonga siku tatu zilizopita ili kwenda kuliosha.

Hakuwa na tabia ya kupika ugali au chakula chochote mara kwa mara nyumbani kwake, ila juzi alifanya hivyo baada ya kununuliwa samaki mkubwa wa kukaanga njiani na rafiki yake.

Pamoja na kwamba aliona hupoteza muda kupika, kula na kuosha vyombo, lakini hakujua kupika.

Hakuwa mjuzi sana wa mambo hayo kwa sababu ya malezi ya utoto kutoka kwao.

Alikuwa mtoto wa kwanza wa kiume, huku wawili waliofuata wakiwa wa kike.

Baba yake alitenganisha kazi. Hakumruhusu kufanya kazi zozote ambazo yeye aliziona za kike, kama vile kupika, kuosha vyombo, kuchota maji na zingine zinazofanana na hizo.

Badala yake zilifanywa na dada zake wawili waliomfuatia kuzaliwa. Hata alipomaliza kula chakula chake mwenyewe, baba yake alimkataza kwenda kuosha walau kikombe alichonywea mwenyewe.

Baba yake alikuwa akimpa kazi ambazo yeye alizitafsiri kuwa za kiume kama vile kufyeka nyasi ndefu zilizozunguka nyumba yao, kwenda kukata migomba iliyokauka kwa ajili ya kuezeka choo, kuchimba mifereji maeneo ambayo maji yametuama kwenye nyumba yao na nyinginezo.

Pamoja na kwamba hayo yote yalimsaidia kwa kuwa mjuzi wa stadi za kazi na kuweza kujimudu kuweza kufanya kazi yoyote, lakini kwa kiasi fulani alimlaumu baba yake kwani ilimsababisha asijue kupika.


Kwa sasa anajitegemea mwenyewe wazazi wake akiwa amewaacha kijijini, akiwa mjini kusaka maisha, lakini mara nyingi alikuwa akila migahawani na kwa mama lishe badala ya kupika.

Na siku akiamua sasa kupika mwenyewe, jiko la mchina linachafuka kwa moshi, huku masufuria yote yakiwa hayatamamiki kwa weusi unaotokana na moshi wa jiko.

Chakula chenyewe inakuwa Mungu nisaidie, wakati mwingine kinaiva, wakati mwingine hakiivi, au kinaungua. Kwa sababu anakula mwenyewe, basi wala haina shida.

Siku ya tatu alikuwa hajaosha sufuria la ugali lililokuwa kwenye meza ambayo ilikuwa imewekewa jiko pia.

Kitu ambacho huwa hasahau siku zote akishamaliza kusonga ugali kwa kubahatisha, ni kuloweka maji sufuria,




**Kwa sasa anajitegemea mwenyewe wazazi wake akiwa amewaacha kijijini, akiwa mjini kusaka maisha, lakini mara nyingi alikuwa akila migahawani na kwa mama lishe badala ya kupika.**

pamoja na kuweka mwiko aliosongea kwenye maji hayo. Alifanya hivyo ili imrahisishie kuosha.

Kitu kilichomfanya aamue kwenda kuosha sufuria ile ni harufu aliyoanza kuisikia wakati anaamka asubuhi.

Ilikuwa kama saa nne hivi, siku ya Jumapili. Ilikuwa ni siku muhimu sana kwake. Ni siku ambayo aliiweka kwenye historia ya kukumbukwa.

Alikuwa ameahidiana na msichana mmoja aliyejitambulisha kwake kwa jina la Nuru. Atakuwa ni msichana wake wa kwanza kuwa naye tangu afike Dar.

Aliahidi angefika hapo majira ya saa 10:00 jioni. Kama isingekuwa harufu aliyoanza kuisikia, sufuria lile na mwiko wake angeweza kuvisukumia uvunguni mwa kitanda chake ili aoshe siku ambayo atakuwa na nafasi.

Ujio na msichana Nuru, ulimpa nguvu wa kusafisha chumba chake na kuamua kuosha sufuria alilopikia, mwiko wa kusongea ugali, pamoja na kusafisha jiko.

Isingewezekana msichana mpya anakuja nyumbani kwake na kukuta kuchafu. Ingeweza kumshushia maksi kwa mpenzi wake huyo.

Alijizoazoa kitandani kivivuvivu, akachukua mswaki wake na kwenda bafuni kuoga. Aliporejea kazi ya kwanza aliyoifanya ambayo hajawahi kuifanya kwa wiki mbili ni kukunja chandarua na kuining'iniza juu.

Siku zote ilikuwa imechomekewa kwenye shuka za kitanda, na alikuwa akitoka na kuingia kupitia eneo dogo analolifunua na kulirudishia, pale anapoingia kulala au kutoka kitandani.

Alipochomoa chandarua na kuikunjakunja kabla ya kuining'iniza, kitu cha pili alichoona muhimu kufanya ni kufagia chumba.

Ni mwezi sasa umepita tangu alipoifanya kazi hiyo, tena kivivuvivu. Alichukua ufagio kibudu, ambao nyasi zake za kufagia zikikuwa zimeishaisha, akaanza kufagia huku akipiga miluzi.

Hakupenda kabisa kufanya kazi hizo, kwa sababu kwao hakuwa anazifanya. Akaanza kumlaumu kimoyomoyo baba yake kwa kumkataza kufanya kazi ambazo alimwambia ni za kike.

"Yaani saa hizi nimekuwa nimeshatandika kitanda, nimefagia, nimeosha vyombo vyote, nikapika chai nikanywa, nikampikia mpenzi wangu chakula kizuri na kitamu," akajisemea mwenyewe kimoyomoyo.

Aliporidhika kuwa amefagia, akaenda sasa kuchukua sufuria la ugali lililojaa maji ya siku tatu zilizopita pamoja na mwiko wake, akatoka nje kwa ajili ya kuosha.

Alichukua na kijiko ambacho alitumia kukwangua ukoko ulioanza kutoa harufu mbaya.

Akamaliza na kuanza kukwangua mwiko. Akajaribu pia kusugua na sufuria lililoanza kuwa jeusi kwa moshi wa tambi za jiko la mchina, ambazo zilikuwa zimepandishwa na kuwasha bila utaalam.

Akaridhika kuwa kila kitu kiko sawa. Akakusanya vyombo vyake akarejea ndani.

Alipoingia tu, akakutana na harufu ile ile. Lakini safari hii iliongezeka kidogo. Ndipo alipogundua kuwa kilichokuwa kikitoa harufu awali, hakikuwa sufuria la ugali lililoachwa kwa siku tatu bila kuoshwa. Kuna kitu kingine ambacho hajakifahamu.

Hakuna na kabati, hivyo sufuria zake alikwenda kuziweka chini ya meza ile ambayo juu yake ilikuwa na jiko, pamoja na vitu vichache vilivyoonekana pale kama kibiriti, chupa tupu ya soda aliyonunua juzi na kuinywa, mshumaa ambao huwasha pale umeme unapozima kutokana na mgawo wa umeme.

Hakuwa mwingine ila ni Heri. Kijana aliyetoka Korogwe mkoani Tanga kusaka maisha jijini Dar es Salaam.

Baada ya kupambana kwa muda mrefu, sasa anaendesha maisha yake kutokana na kuuza viatu vya mitumba pale kwenye kituo cha Chanika.

Hufanya kazi hiyo jioni na usiku, kwa kutandika turubai kando ya barabara na kuvimwaga, kabla ya kuitia wateja.

Kazi hii angalau ilimwingizia kipato cha kujikimu mwenyewe, ikiwa ni pamoja na kuweza kulipia kodi ya nyumba, kula na kuvaa kwa kiasi alichojaaliwa. Alipanga chumba kimoja.

Chumba chake kilikuwa cha uani, kikiwa moja kati vyumba vitatu vilivyokuwa uani, vilivyounganishwa kwenye safu moja, na mbele yake kubebwa na nyumba kubwa nyingine ya vyumba sita, maeneo ya Chanika.

Ilishatimu saa sita kamili mchana na katika kunusa aligundua kuwa harufu ile haikuwa ya kitu kingine zaidi ya panya aliyekufa.

Hapo aliona sasa kuna kazi kubwa ya kufanya. Nayo ni kumsaka panya huyo na kumtoa ili mpenzi wake akiwasili asikutane na harufu hiyo kwani ni aibu kubwa.

Hakukuwa na kingine chochote zaidi ya kupekua chumba chote ili kumsaka, ingawa kwa anavyojua haitokuwa kazi rahisi.

ITAENDELEA JUMAPILI




# H BABA ATOA MSAADA WA BAISKELI

MSANII mkongwe wa Bongo Fleva, H Baba, amezidi kuonyesha upendo kwa watu wasiojiweza, baada ya kutembelea na kumkabidhi baiskeli ya walemavu, mkazi mmoja wa Mbezi Africana, mkoani Dar es Salaam.

Akizingumza wakati akikabidhi baiskeli hiyo, H Baba alisema lengo sio kutangaza misaada anayotoa, bali ni kuhamasisha wasanii wengine kukumbuka kuwasaidia watu wanaohitaji misaada.

"Kutoa ni moyo na sio utajiri, kidogo tulichonacho tunapaswa kuwapa furaha wahitaji, ninashukuru kampuni zote ambazo zimenipa ubalozi kwa kuniwezesha kumsaidia ndugu yangu," amesema H Baba.

Aliwashukuru wadau wake kama Sharobaro wa Insta na Sodox kwa kumuwezesha nguo na fedha ambazo zote amemkabidhi mkazi huyo.

"Kwa kipekee namshukuru Diamond Platnumz, Kharas, Iham, Dicksound na Lonely Nzali kwa kuniunga mkono katika jambo hili," ameongeza H Baba.

# REMA HASHIKIKI TENA

MWANAMUZIKI Nyota wa Nigeria, Rema amezidi kupata mafanikio baada ya albamu yake inayoitwa Rave & Roses, kufikiwa kiwango cha Platinum nchini Ufaransa.

Albamu hiyo ni ya pili kwa muziki wa kiafrika kufikia hadhi hiyo ndani ya taifa la Ulaya.

Ndani ya albamu hiyo kuna nyimbo mbalimbali zenye ladha mbalimbali ya muziki kama Afro-rave, dancehall na nyimbo za Kiarabu.

Kufikia hadhi hiyo kubwa imechochewa na nyimbo maarufu kama vile Calm Down ambayo ilifika nambari tatu kwenye Chati ya Singles ya nchini Uingereza na baadaye kushika nafasi ya kwanza kwenye Billboard Hot 100 ya Marekani baada kurudiwa tena akimshirikisha Selena Gomez.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**UNITED YAMTAKA OMLO**
KLABU ya Manchester United imeingia katika kinyang'anyiro cha kumsajili mchezaji wa kimataifa wa Hispania, Dani Olmo, ambaye ana kipengele cha pauni milioni 52 kuondoka RB Leipzig msimu huu. Winga huyo mwenye umri wa miaka 25 pia anazivutia Real Madrid, Manchester City, Chelsea na Tottenham. **(Daily Mail)**

**JOSELU ANUKIA UNITED**
WAWAKILI wa Manchester United wamekwenda Hispania kuwasaka wachezaji wapya akiwamo mshambuliaji, Joselu, mwenye umri wa miaka 24, ambaye anacheza kwa mkopo Real Madrid kutoka Espanyol, ni miongoni mwa majina kwenye orodha yao. (**Relevo**)

**DAU LA BREMER LATAJWA**
MANCHESTER United italazimika kulipa angalau euro milioni sita ili kumnunua mchezaji wa kimataifa wa Brazil, Gleison Bremer, mwenye umri wa miaka 27 ambaye anaichezea Juventus na mshambuliaji wa Mashetani Wekundu, Mason Greenwood (22), anaweza kujumuishwa katika mpango huo. (Gazetta dello **Sport)**

**BRATHWAITE AGOMBEWA EPL**
MANCHESTER City na Newcastle United zitachuana na Manchester United katika kumsajili beki wa kati wa Everton na England wa kikosi cha umri wa chini ya miaka 21, Jarrad Brathwaite. (**Football Transfers**)

**GUDMUNDSSON AWEKWA SOKONI**
KLABU ya Italia ya Genoa inatarajia kupokea ofa msimu wa joto kwa mshambuliaji wa Iceland, Albert Gudmundsson, mwenye umri wa miaka 26, ambaye amekuwa akihusishwa na Tottenham Hotspur na West Ham. **(Fabrizio Romano)**

**RAPHINHA ATAJWA NEWCASTLE**
NEWCASTLE United iliwafuatilia wachezaji kadhaa wa Brazil wakati wa mechi yao ya kirafiki dhidi ya England wiki iliyopita, huku winga wa Barcelona, Raphinha mwenye umri wa miaka 27 na mlinzi wa Juventus, Gleison Bremer (27), wakiwa kwenye darubini yao. (**Newcastle Chronicle**)

**LUKAKU ANUKIA SAUDIA**
KUNA kishawishi kikubwa kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 30, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo AS Roma akitokea Chelsea kuhamia Saudi Arabia. **(Calcio Mercato)**

**UNITED, SPURS VITANI**
MANCHESTER United na Tottenham Hotspur zinamwania, Jean-Clair Todibo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24, ambaye anaweza kupatikana kwa dau la pauni milioni 40 kutoka Nice msimu huu wa joto.**(Talksport)**

**MOSQUERA AGOMBEWA ULAYA**
KLABU ya Crystal Palace inataka kumsajili mlinzi wa Valencia mwenye umri wa miaka 19, Cristhian Mosquera, ifikapo msimu wa joto, lakini watakabiliana na ushindani wa kumnunua mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania kutoka Atletico Madrid. (**Evening Standard)**

**ADAMS KUTUA WOLVES**
KLABU ya Wolves inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mshambuliaji wa Southampton na Timu ya Taifa ya Scotland, Che Adams, mwenye umri wa miaka 27, atakapokuwa mchezaji huru msimu wa joto. **(Telegraph**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA: ARSENAL INA NAFASI KUITIKISA CITY

## ●●● Pia aweka wazi kwake Guardiola ndiye kocha bora duniani katika...

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amemsifu Pep Guardiola kama "kocha bora zaidi duniani kwa maili moja" lakini anaamini Arsenal wanaweza kutoa kauli ya ushindi dhidi ya Manchester City ili 'kutikisa' mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England, timu hizo zitakapokutana leo.

Arsenal hawajashinda katika mechi nane walizotembelea kwenye Uwanja wa Etihad kuanzia Januari 2015, wakipoteza mara saba huku wakichapwa mabao 4-1 Aprili, mwaka jana.

Urafiki wa muda mrefu wa Arteta na Guardiola unajumuisha miaka mitatu ya kufanya kazi pamoja akiwa msaidizi wake City kabla ya kuchukua usukani wa Arsenal mnamo Desemba, mwaka 2019.

"Pongezi zangu na kile ninachohisi kwake hakika hakijabadilika," alisema Arteta.

"Kwa maoni yangu yeye ndiye kocha bora zaidi duniani kwa maili moja na ni mmoja wa watu wazuri ambao nimekutana nao kwenye soka.

"Hakika yeye ni mmoja wa wale ambao nimekuwa na furaha na kicheko zaidi kufanya nao kazi. Hiyo itakaa kwangu milele.

"Tumejitahidi sana kuwa katika nafasi tuliyopo, lakini tunatakiwa kwenda siku baada ya siku, tufanye mazoezi vizuri, tujiandae kila mechi. Tumefanya mengi ili tuwe hapa tulipo sasa tunatakiwa kukumbatia nafasi hiyo na kwenda kwa ajili yake.

"Lazima uchukue hatua kali ili kuwa hapo na nadhani tumefanya makubwa katika misimu ya hivi karibuni. Tunakaribia zaidi na sasa ni jinsi gani tunaziba pengo hilo na kujaribu kuwa bora zaidi yao."

Arsenal walikuwa na faida ya pointi nane dhidi ya City mapema Aprili msimu uliopita na kushinda mechi mbili pekee kati ya tisa za mwisho, ikiwa ni pamoja na sare dhidi ya Liverpool, West Ham na Southampton huku timu ya Guardiola ikitwaa taji lao la tano katika misimu sita.

Akitafakari jinsi ya kuepuka hali kama hiyo wakati huu ambapo timu yake inaiongoza Liverpool kileleni mwa jedwali kwa tofauti ya mabao, Arteta alisema: "Kuna wakati unapokuwa Anfield na uko mbele kwa mabao 2-0 na unashindwa.

"Tulipata majeraha, kulikuwa na mchezo wa Sporting (kwenye Ligi ya Europa katika hatua ya 16 bora) na kulikuwa na sababu nyingi. Kisha kasi ikabadilika na kuwa mbaya na tulijitahidi kuendelea kwa sababu waliendelea kushinda. Walishinda 14 au 15 mfululizo!

"Jumapili ni mchezo mkubwa kwa timu zote mbili. Utatupa nguvu kubwa tena ikiwa tutaenda huko na kuushinda. Bado kuna safari ndefu, ndefu na ndefu ya kufanya uwanja wa kushinda."

Arteta alithibitisha Bukayo Saka (msuli wa paja), Gabriel Martinelli (mguu) na Gabriel Magalhaes (kifundo) wote wanaweza kucheza dhidi ya City.

# XAVI KUWASHTAKI WAANDISHI WA HABARI



**BARCELONA,** Hispania

KOCHA wa Barcelona, Xavi Hernandez alithibitisha atachukua hatua za kisheria dhidi ya wanahabari wawili ambao alisema walitengeneza habari kumhusu yeye.

Taarifa ziliibuka wiki hii zikidai Xavi hakufurahishwa na ripoti moja iliyosema alidai aliwataka makocha wote wa timu yake kuweka simu zao mezani ili abaini nani anavujisha siri za klabu hiyo.

Habari nyingine ilihusu mwandishi wa habari ambaye alidai Xavi alimtumia ujumbe akilalamika kuhusu ukosoaji aliochapisha, ambao ulikanushwa na vyanzo vya karibu na bosi wa Barca.

"Ninaelewa ukosoaji lakini kuna mipaka," alisema Xavi katika mkutano na waandishi wa habari kabla ya mchezo wa LaLiga dhidi ya Las Palmas uliochezwa kwenye Uwanja wa Olimpiki jana.

"Sitavumilia uongo au watu kubuni vitu. Ni wakati wa kusema vya kutosha, ni uongo mkubwa, kwa hiyo sasa ni wakati wa kuchukua hatua."

Xavi amevikosoa vyombo vya habari mara kadhaa msimu huu, akipendekeza Disemba vyombo vya habari hasi vilikuwa vinaathiri uchezaji wa timu yake.

Baada ya kufika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi huu, alitaja na kushutumu makala ya Desemba ambayo ilisema Barca ilikuwa na "mzaha" wa mashindano haya ya Ulaya.

Mazingira makali ya vyombo vya habari yanayoizunguka klabu hiyo yalikuwa moja ya sababu zilizochangia Januari kutangaza atajiuzulu mwishoni mwa msimu huu.

Tangu wakati huo, Barca hawajafungwa katika mechi 10, na kutinga hatua ya nane bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu 2020 na kupanda hadi nafasi ya pili kwenye LaLiga, ingawa wamepitwa alama nane nyuma ya vinara Real Madrid.

Imesababisha wito kwa Xavi, ambaye aliiongoza Barca kutwaa ubingwa wa LaLiga msimu uliopita, kusitisha uamuzi wake na kujitolea kuinoa timu hiyo ya Katalunya mwakani.

"Ninashukuru watu wanataka nibaki, lakini hakuna kilichobadilika, ninafikiria maslahi ya klabu," aliongeza.

Kiwango cha hivi karibuni cha Barca kilichangiwa na kuibuka kwa Lamine Yamal na Pau Cubarsí, ambao wana umri wa miaka 16 na 17 na tayari ni wachezaji wa kimataifa wa Hispania.

Mshambuliaji Yamal alilipa taifa lake sare ya 3-3 Jumanne dhidi ya Brazil, akipokea pongezi kutoka Santiago Bernabéu.


# Madrid yamfuatilia Alexander-Arnold

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inafuatilia hali ya Trent Alexander-Arnold ndani ya Liverpool anapokaribia miezi 12 ya mwisho ya mkataba wake, kwa mujibu wa 90min.

Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 25, bado hajaanza mazungumzo ya mkataba mpya na Liverpool, ambao kipaumbele chake katika miezi michache iliyopita kimekuwa ni kutafuta uongozi mpya wa michezo na kumteua kocha mpya kufuatia uamuzi wa Jurgen Klopp kujiuzulu mwishoni mwa msimu huu.

Michael Edwards amerejea katika Kundi la Fenway Sports kama Mkurugenzi Mtendaji wa Soka, jukumu ambalo litamfanya apewe madaraka katika shughuli za kila siku hapo Liverpool, wakati Richard Hughes



atakuwa mkurugenzi mpya wa michezo msimu huu wa joto.

Lakini utafutaji wa kocha mpya unaendelea baada ya Xabi Alonso kutangaza hataondoka Bayer Leverkusen mwaka 2024.

Kutokujua utambulisho wa kocha anayefuata inafahamika moja ya sababu kuu za kucheleweshwa kwa mazungumzo ya mkataba wa Alexander-Arnold, huku beki huyo wa kulia akitamani kuelewa ni nini kocha mpya amepanga kwa ajili yake, ikiwa ni pamoja na nafasi ambayo atacheza.

Muhimu zaidi, hakuna mvutano kati ya Alexander-Arnold na Liverpool, kwani pande zote mbili zimekuwa wazi kuhusu hali zao na mazungumzo ya mkataba yakipangwa mara tu Liverpool watakapomtambua kocha mpya.

Hata hivyo, huku Alexander-Arnold akiwa bado hajahakikishiwa kubaki na Liverpool, Real Madrid wameongeza nia yao katika hali hiyo.

Akionekana kama mtu mwenye kipaji cha hali ya juu ambaye anaweza kupatikana kwa ada ya manunuzi iwapo mazungumzo na Liverpool yatavunjika.

Nia ya Madrid kwa Alexander-Arnold inakuja baada ya ripoti za muda mrefu za kutaka kumsajili Reece James wa Chelsea kuonekana ngumu.

James hajawahi kuonyesha nia ya kutaka kuondoka Chelsea na anaendelea kujituma kikamilifu na kuchukua unahodha wa klabu.

# Alonso: Siondoki Bayern Leverkusen

**DORTMUND,** Ujerumani

XAVI Alonso amethibitisha kubakia Bayer Leverkusen kwa msimu wa 2024-25 licha ya timu kubwa za Ulaya zikiwamo Bayern Munich na Liverpool kumwinda na kusema klabu hiyo ndiyo sehemu bora zaidi kwake kuendeleza maendeleo yake kama kocha.

Alonso, ambaye anaiongoza Leverkusen kuelekea kutwaa taji la Ligi Kuu Ujerumani (Bundesliga), aliuambia mkutano na waandishi wa habari alitumia mapumziko ya kimataifa kufikiria chaguo lake na kufikia uamuzi wake mwenyewe.

"Umekuwa msimu wenye uvumi mwingi kuhusu mustakabali wangu," alisema Alonso.

"Nilitaka kutumia mapumziko ya kimataifa kutafakari vizuri zaidi na kuchukua uamuzi.

"Wiki iliyopita nilikuwa na mkutano mzuri na Simon (Rolfes, Mkurugenzi wa Michezo wa klabu) na Fernando (Carro, Mkurugenzi Mtendaji), na nilijulisha uamuzi wangu wa kuendelea kuwa kocha wa Bayer Leverkusen.

"Kwa hakika maamuzi yote, unahitaji kuchambua vizuri, na nilijaribu kuchukua yale sahihi, nilijaribu kuchukua yale ambayo yanakuja kwa njia ya asili, na kwa sasa ninahisi hii ndio mahali sahihi kwangu kujiendeleza kama kocha.

"Mimi ni kocha mchanga, lakini lazima nijisikie, na hivi sasa ninahisi hapa ndio mahali pazuri."

Juzi vyanzo viliiambia ESPN Liverpool waliachana na mpango wa kumteua kiungo wao wa zamani kama mrithi wa Jurgen Klopp, wakati rais wa heshima wa Bayern, Uli Hoeness, alisema kumwajiri Alonso msimu huu wa joto "labda haiwezekani."

Sifa ya Alonso kama kocha imekua haraka tangu kuteuliwa kwake pale BayArena mnamo Oktoba 2022 -- haswa msimu huu, ambapo timu yake bado haijapoteza katika rekodi ya Ujerumani ya mechi 38 na inaonekana uwezekano wa kumaliza ushujaa wa miaka 11 wa Bayern Munich kwenye Bundesliga.

"Ni mchakato, maendeleo ya timu ni sambamba na maendeleo yangu kama kocha," aliongeza.

"Huu ni msimu wangu wa kwanza kamili kama kocha. Bado nina mambo mengi ya kuthibitisha mwenyewe, uzoefu, na hivi sasa nina hali katika klabu ambayo ninahisi utulivu, mwenye furaha na timu na klabu."

HABARI MICHEZO

# SIMBA: HATUJAKATA TAMAA KUTINGA NUSU FAINALI CAF

**Na Shufaa Lyimo**

LICHA ya kupoteza mchezo wa kwanza ikiwa nyumbani, uongozi wa Simba umesema bado una matumaini ya kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika yanayoendelea.

Simba ilikubali kufungwa bao 1-0 na Al Ahly katika mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi usiku.

Akizungumza na gazeti hili mara baada ya mechi hiyo kumalizika,Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema licha ya kufungwa bao moja, lakini wachezaji wao walionyesha kiwango kizuri na walipambana.

Ahmed alisema wachezaji wao walipata nafasi nyingi za kufunga mabao lakini walishindwa kuzitumia vyema na kupelekea kupoteza mchezo huo.

"Simba huwa hatupendi kukata tamaa mapema, tunaamini bado tuna nafasi ya kufanya vizuri katika mchezo wetu ujao wa marudiano utakaochezwa Misri, kila mmoja aliona jinsi tulivyocheza," alisema Ahmed.

Aliongeza kwa sasa wanakwenda kufanya marekebisho kwa sababu bado malengo yao ni kuingia hatua ya nusu fainali katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hayajapotea.

Aliongeza mpinzani wao alipata nafasi moja na alifanikiwa kuitumia, hivyo aliondoka na ushindi akiwa ugenini.

"Tutakwenda Misri tukifahamu lolote linaweza kutokea katika mchezo wetu huo, tunaomba mashabiki na Watanzania waendelee kutuombea ili tusonge mbele, " alisema meneja huyo.

Pia aliwashukuru mashabiki wao kwa kujitokeza kwa wingi uwanjani kwa lengo la kuwaongezea hamasa wachezaji.

Al Ahly itaikaribisha Simba katika mchezo wa marudiano utakaochezwa Aprili 5, mwaka huu jijini Cairo, Misri.




Mchezaji wa timu ya Mipango Veteran, Emannuel Jastine (katikati), akimiliki mpira huku akizongwa na wachezaji wa timu ya Polisi Veteran katika mchezo wa kirafiki uliochezwa kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Al Ahly yavunja rekodi ya Simba

INATOKA UK. 24

"Tumecheza dhidi ya timu kubwa, tumefanya kosa moja wametufunga, wamepata nafasi moja wameitumia, kwa ujumla tumecheza mechi nzuri na tumecheza vizuri, lakini hatukufunga. Kama hufungi huwezi kushinda, lakini tuna mechi ya marudiano, hatuna cha kupoteza.

Katika mechi kubwa hizi huwezi kupata nafasi nyingi kama hizi, niombe radhi ya mashabiki kwa sababu kama hakuna matokeo mazuri ni tatizo. Niseme tu tuna matatizo, kama wachezaji wanaingia ndani ya eneo la hatari mara saba na mnashindwa kufunga ni tatizo," Benchikha alilalamika.

Aliongeza wachezaji wake walipambana na wamejaribu kucheza vizuri dhidi ya vigogo hao wa Afrika.

"Wachezaji wote wamecheza vizuri, Ngoma (Fabrice), Ntibazonkiza (Said), Kibu (Dennis), wachezaji wote wamecheza vizuri. Kuna mchezo wa pili, hatuna cha kupoteza tunajiandaa kucheza mchezo wetu mkubwa, na leo (juzi), wachezaji wangu wamekuwa na mchezo mzuri, unapochezea dhidi ya timu kubwa, tumeruhusu bao dakika za mwanzoni," alisema Benchikha.

Naye aliyekuwa Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, alisema wamecheza mpira mzuri lakini bao la mapema walilopata Al Ahly lilimaliza mchezo.

"Kwa jinsi tulivyocheza, tumemiliki mpira na kutengeneza nafasi zaidi ya sita lakini tatizo ni umakini wa washambuliaji kushindwa kufunga, ninaimani kubwa ndani ya siku tatu hizi benchi la ufundi litafanyia kazi na kwenda Misri kwa matumaini makubwa," alisema Mgunda.

Makamu wa Rais wa Yanga, Arafat Haji, alisema anaona nafasi kubwa ya timu zote za Tanzania kutinga hatua ya nusu fainali, licha ya Simba kupoteza mchezo wa nyumbani. "Mpira ni mchezo wa makosa, hii mechi hajapoteza Simba pekee, Tanzania kwa sababu ilikuwa uwanjani kuipeperusha bendera ya nchi, ninaimani nao wanaenda kufanya maajabu Misri, na timu zote zinaweza kwenda nusu fainali," alisema bosi huyo wa Yanga.

Kocha Mkuu wa Al Ahly, Marcel Koller, alifurahi kwa ushindi na alifahamu mchezo huo utakuwa mgumu kutokana na baadhi ya wachezaji wametoka katika majukumu ya timu za taifa na wakalazimika kusafiri moja kwa moja bila kupata muda wa kupunzika.

"Mchezo ulikuwa mgumu, huu umeisha na sasa tunahamisha macho yetu mchezo wa marudiano, utakuwa mgumu na tofauti kwa sababu bado hatujashinda, tunaongoza tu," alisema Koller.

## Onesmo atamba kutoa kichapo

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA chipukizi, Lucas Onesmo, amesema anaamini ataibuka mshindi dhidi ya mpinzani wake, Said Faraji, katika pambano lao 'Hatukimbii Hatuogopi' litakalofanyika siku ya Eid Pili mkoani, Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Onesmo, alisema anaendelea vyema na maandalizi kuelekea pambano hilo huku akitamba atamaliza mapema mchezo huo.

Bondia huyo alisema amejipanga kumchapa mpinzani wake mapema katika raundi ya kwanza.

"Hili pambano dhidi ya Faraji haliniumizi kichwa, nitamchapa, yeye anasema kichwa chake hakina ubongo, sasa mimi nataka nimrudishie ili awe timamu, nitampa adhabu ambayo hataisahau, " alisema Onesmo.

Aliongeza mpinzani wake hana uwezo wa kumpiga kutokana na maandalizi anayofanya na kikubwa anataka kuwapa burudani mashabiki wake.

Naye Kocha Mkuu wa Onesmo, Fadhili Kambi, alisema hana shaka na bondia wake kutokana na mazoezi anayompa.

"Ninawaahidi mashabiki wetu tutakwenda kumpiga mpinzani, aingie ulingoni kwa tahadhari, ubongo wake tuliuchukua sisi maana huwa anasema hana ubongo," alisema Kambi.

## Yanga SC haikamatiki nyumbani, ugenini

INATOKA UK. 24

mechi nyingi kila timu ikiwa imeshinda michezo 14 mpaka sasa.

Yanga mpaka sasa inaongoza kwa kufunga mabao mengi kwenye ligi hiyo, ikiwa na magoli 49, lakini ikifuatiwa kwa karibu na Azam FC, ambayo yenye mabao 47 mpaka sasa.

Hata hivyo, Yanga ina mchezo mmoja pungufu ukilinganisha na Azam ambayo imeshacheza michezo 21.

Yanga imetoa sare moja tu mpaka sasa, Simba ikiwa na sare tatu na Azam tano.

Takwimu pia zinaonyesha Yanga imeshinda michezo yote 12 iliyocheza nyumbani, huku nane ikicheza ugenini ikifanya idadi ya mechi zake kuwa 20.

Katika mechi nane ilizocheza ugenini, imeshinda mechi tano, imepoteza mbili na sare moja.

Hata hivyo, timu hiyo imepoteza mechi mbili sawa na Simba na Azam ambazo zote zimepoteza idadi sawa za mechi.

# Michezo

Jumapili Machi 31, 2024

Nipashe




## Alonso: Siondoki Bayern Leverkusen

UKURASA 22



Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis (kushoto), akijipanga kumtoka beki wa Al Ahly kutoka Misri katika mechi ya hatua ya robo fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi usiku. Simba ilifungwa bao 1-0. **PICHA: SIMBA SC**

# AL AHLY YAVUNJA REKODI YA SIMBA

## ●●● Benchika alia na washambuliaji wake, afunguka bao la mapema...

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

WAKATI ushindi wa bao 1-0 walioupata Al Ahly kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi usiku umehitimisha rekodi nzuri ya Simba nyumbani, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Abdelhak Benchikha, amesema washambuliaji wake walimwangusha katika mechi hiyo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba juzi imepoteza mechi ya kwanza ya mashindano ya kimataifa dhidi ya Waarabu hao kutoka Misri.

Lilikuwa ni bao la dakika ya nne likifungwa na Ahmed Nabil Koka, lilihitimisha rekodi nzuri ya Simba, lakini pia likiiweka katika nafasi ngumu kuelekea mechi ya marudiano ya robo ya michuano hiyo itakayochezwa Ijumaa kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Cairo.

Simba ilikuwa haijawahi kupoteza mechi yoyote dhidi ya Al Ahly ikicheza nyumbani, lakini rekodi hiyo ilifikia kikomo juzi baada ya michezo tisa, tangu zilipokutana mara ya kwanza mwaka 1985.

Simba ilianza kucheza na Al Ahly Agosti 22, 1985 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza ikashinda mabao 2-1, ikiwa ni michuano ya Kombe la Washindi Afrika, sasa Kombe la Shirikisho, lakini ikatolewa kwa kufungwa magoli 2-0 ugenini, mechi ikifanyika Agosti 29, mwaka huo.

Februari 2, mwaka 2019 katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi, Simba ilifungwa mabao 5-0 ugenini, kabla ya kushinda goli 1-0 nyumbani, siku 10 baadaye.

Simba ilishinda tena nyumbani dhidi ya Al Ahly bao 1-0 hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa, Februari 23, mwaka 2021, lakini ikaenda kufungwa bao 1-0 ugenini Aprili 9, mwaka huo.

Kwa mara ya kwanza Simba ilitoa sare nyumbani ya mabao 2-2 dhidi ya Al Ahly, Oktoba 20, mwaka jana kwenye michuano ya African Football League, ikapata sare ya kwanza ugenini dhidi ya timu hiyo (1-1), Oktoba 24, mwaka jana.

Baada ya mechi hiyo kumalizika juzi, Benchikha alisema licha ya kufurahia kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji wake, lakini alilalamika kukosa mabao saba ya wazi katika mchezo huo.

INAENDELEA UK 23

# Yanga haikamatiki nyumbani, ugenini

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumaliza dakika 90 za nyumbani za mechi ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Mamelodi Sundowns kutoka Afrika Kusini, Yanga imeweka rekodi nne kwenye Ligi Kuu Bara ambayo ilisimama kupisha kalenda ya michezo ya kimataifa.

Ikiwa inaongoza katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kujikusanyia pointi 52, Yanga ndiyo timu inayoongoza kwa kushinda mechi nyingi zaidi, ikitoa sare chache, timu yenye mabao mengi, lakini pia imeshinda mechi zote ilizocheza kwenye uwanja wa nyumbani.

Kwa mujibu wa takwimu za dawati la michezo la Nipashe, Yanga imeshinda michezo 17 ambapo hakuna timu yoyote mpaka sasa iliyoshinda idadi hiyo ya michezo.

Timu hiyo imeshinda idadi hiyo ya michezo ikiwa imecheza mechi 20 tu, hivyo ni mechi tatu tu ambazo haikupata ushindi.

Mechi hizo ni zile mbili ilizopoteza dhidi ya Ihefu FC, ikifungwa mabao 2-1 kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Oktoba 4, mwaka jana, mechi ya mzunguko wa kwanza na nyingine ni Machi 17, mwaka huu ilipofungwa mabao 2-1 dhidi ya Azam FC, Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Yanga imepata suluhu mechi moja dhidi ya Kagera Sugar, Februari 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kaitaba ulioko Bukoba, Kagera.

Simba na Azam zinafuatia kwa kushinda

INAENDELEA UK 23



9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042